

YESU KRISTO YEYE YULE

JANA, LEO, NA HATA MILELE



Mu hali gani? Mwaweza kuketi. Haya hakika ni majaliwa kurudi tena, usiku wa leo, huku Beaumont, Texas. Tangu nilipokuwa hapa mara ya kwanza, daima nimetamani kurudi tena kuhudumu na kushirikiana kwenye Neno la Mungu pamoja nanyi watu wapendwa, tena, kamwe hamkutoka moyoni mwangu. Ninaweza kukumbuka mambo mengi makuu yaliyotukia wakati wa mwisho nilipokuwa hapa Beaumont. Kwa hiyo, ninaamini imekuwa yapata miaka kumi na miwili iliyopita, karibu hiyo.

² Ninakumbuka kulikuwako, hao watu, ndio kwanza tuwe na mkutano mkubwa huko Houston. Halafu nikaninii... Au nilitoka hapa kwenda Houston? Hapa, kutoka Houston, hapa. Na hapo ndipo Malaika wa Bwana aliposhuka, wakampiga picha. Na ni ninii tu... Nafikiri wana picha kama sita ama nane za Hiyo tangu wakati huo, mwajua, mahali mbalimbali, tatu huko Ujerumani hivi majuzi tu. Wana moja ya rangi ya *Kodakromu*, huko juu, mahali fulani kwenye uwanja wa maonyesho huko California, Lakeport, California, ambako Wafanyabiashara Wakristo walikuwa... Ni, kwa kweli, picha nzuri ya Uwepo Wake, ule Moto wa kaharabu ukiwaka kote.

³ Hii, bila shaka, ilipigwa isiyo na rangi, nayo inaonekana tu kama nyeupe, lakini kwa kweli ni Nuru ya kaharabu. Na kama vile nimesema sikuzote tangu, kama mmoja wa hawa vijana hapa, ilikuwa ni, nilisema manjano-ya-kijanikibichi. Sikujua *kaharabu* ilikuwa nini, kwa hiyo nikasema tu manjano-ya-kijanikibichi.

⁴ Niliposikia hivi majuzi hao wavulana walikuwa—walikuwa wakiomba, na, kuhusu kwamba tupitie njia gani tulipoanza mwanzoni mwa mwaka, basi mahali pa kwanza palipoingia moyoni mwangu palikuwa ni Beaumont, Texas. Nikasema, “Je, una marafiki wowote?”

Akasema, “Kadhaa.”

⁵ Nikasema, “Anza kuwapigia simu basi. Tutaanzia huko, ndipo tuone tu mahali ambapo Bwana atatuongoza.” Huu ndio mkutano wetu wa kwanza baada ya—ya mwanzo wa mwaka.

⁶ Muda mfupi uliopita, niliambiwa na mwanangu, nasi tukaja pamoja na bintiye Ndugu Jack Moore kutoka hotelini, ama moteli, hasa, walikuwa wakizungumza, nami ninaamini Billy aliniambia ya kwamba huyo ndugu, mchungaji wa kanisa hili, sijawahi kukutana naye, isipokuwa huyo ndiye niliyepeana naye

mikono papa hapa, ambaye alikuwa akiomba kwa miaka mingi turudi Beaumont.

⁷ Loo, kamwe si—sitajua jinsi ya kuwathamini marafiki waaminifu kama hao mpaka tutakapovuka mto, wakati mwingine, mtu anayeamini kiasi hicho katika huduma ambayo Bwana Yesu alinipa. Si ajabu nisingeweza kuwazia jambo lingine ila Beaumont wakati huu. Maombi hubadilisha mambo.

⁸ Nami nikasikia ya kwamba kulikuwa na ndugu mwingine aliyeungana naye katika maombi ambaye ameenda Utukufuni. Billy alikuwa akiniambia habari zake dakika chache zilizopita, wakati mimi na Jack, na yeye tukishuka kutoka hotelini. Vema, hapana shaka usiku wa leo, katika Nchi bora kuliko hii ilivyo, hana budi kujua habari zake.

⁹ Ninaamini ya kwamba—ya kwamba mtu anapokufa ananinii tu, *kifo* maana yake ni, “utengano,” yeye hutenganishwa tu tusimwone, bali daima yu hai. “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Loo, ni—ninaamini hilo!

¹⁰ Hatuwezi kufa, tunao Uzima wa Milele. Milele, chochote ambacho ni cha Milele kamwe hakikuwa na mwanzo wala mwisho, kwa hiyo huo ni Uzima wa Mungu Mwenyewe. Uzima wa Milele unatokana na neno la Kiyunani hapo, *Zoe* ambalo linamaanisha, “Uzima wa Mungu Mwenyewe” uko ndani yetu. Basu tunapokuwa wana na binti za Mungu, basi tunaishi kama tu Mungu aishivyo, hatuwezi kufa zaidi ya vile Yeye anavyoweza kufa, kwa hiyo sisi ni sehemu Yake. Hivi hamna furaha kuwa wana na binti za Mungu? Ni jambo zuri jinsi gani!

¹¹ Mnajua nafikiri baadhi ya mikutano bora sana tuliyopata kuwa nayo ni makanisani. Sasa, ninapenda . . . Wakati mwingine mikutano, mwajua, inafikia mahali ambapo sisi, umati ni mkubwa, hatuwezi kuingia kwenye, kwenye makanisa madogo, na kadhalika, ama makanisa makubwa, lakini kuna jambo *fulani* kuhusu nyumba ya kanisa. Sasa natumaini hamtafikiri ya kwamba nimeingia katika vurumai fulani tangu nilipowaona mara ya mwisho, lakini, mwajua, ninaamini ya kwamba mahali fulani, kanisa, ndipo Mungu anapokaa, Malaika wanaishi miongoni mwa makanisa, ni mahali palipowekwa wakfu kwa ajili ya utumishi wa Mungu.

¹² Huko nje kwenye kumbi hizi za mikutano, na kadhalika, tunaona wana karamu, dansi, unywaji pombe, na kila kitu, nawe unahisi ro—roho ambayo haionekani kuwa sawa. Inaonekana tu kana kwamba ni . . . Na, vinginevyo, Roho Mtakatifu daima huonekana akifanya kazi tofauti sana mnapokuwa kanisani, mnajua, mahali fulani, hasa sana katika kanisa zuri, lililojazwa na Roho, ambapo watu wamejazwa na Roho Mtakatifu, na ishara

kuu na maajabu yanatukia, nao watu wanaoamini mambo haya kuwa ni kweli.

¹³ Watu ndio kanisa. *Kanisa* ni neno linalomaanisha, “walioitwa watoke.” Ni kundi la watu walioitwa kutoka ulimwenguni wapate kutembea pamoja na Mungu, hilo ndilo kanisa. Nina furaha sana kuwa mmoja wa hao, usiku wa leo. Kama ningekuwa na maisha mia moja ya kuishi, na hakukuwa na maisha ya baadaye baada ya mimi kufa, bado ningetaka kuishi kila moja ya hayo kwa ajili ya Yesu Kristo, hiyo ni kweli, mimi, inamaanisha hivyo kwangu.

¹⁴ Ndugu Jack alikuwa akinionyesha lile tangazo, nilisimama na kanisa lake jana usiku, tukishuka, kanisa zuri sana, la kiroho huko Shreveport, Louisiana, naye alikuwa akinionyesha picha aliyokuwa ameweka kwenye gazeti nilipokuwa huko miaka kadhaa iliyopita, badiliko kubwa mno, mtu asingejua alikuwa ni mtu yule yule. Lakini kuna *namna fulani au nyingine* katika mwili huu wa kibinadamu ambapo tunazeeka na kuoza, hivyo tu, lakini roho zetu zinabaki vile vile, wala haziwezi kufa.

¹⁵ Nilisema jana usiku kwenye kanisa la Ndugu Jack, nilisema, “Kama tungeweza kuelewa, *huu* ni mkono wangu, *hiki* ni kidole changu, *hili* ni sikio langu, *hii* ni pua yangu, *haya* ni macho yangu, lakini *mimi* ni nani? *Mimi* ni nani ninayemiliki hili? *Hili* si *mimi*, *hiki* ni kitu ninachomiliki.” Mnaona, wewe ni roho, kamwe hamjawahi kuniona *mimi*, mnaona kilicho changu kinachonitangaza *mimi*, bali hamjawahi kuniona *mimi*.

¹⁶ Kama vile Biblia ilivyosema, “Hakuna mtu aliyewahi kumwona Mungu wakati wowote, bali Mwana wa pekee atokaye kwa Baba amemfunua.” Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha Ulimwengu kwa nafsi Yake. Waliona kile Mungu alichokuwa, maana Yeye alijidhihirisha Mwenyewe kupitia Kristo, maana Yeye alikuwa na Utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili, angeweza kumdhihirisha *Yeye*.

¹⁷ Lakini sasa, na basi kwa kuwa sisi ni wana na binti za Mungu, na warithi pamoja Naye katika ule Ufalme, basi tunamdhihirisha Yeye maishani mwetu. Wakati mwingine, kama—kama wengi wetu tungeishi tu mahubiri yetu badala ya kuyahubiri, nafikiri ingekuwa—ingekuwa bora zaidi, kama tukiendelea tu na kuyaishi hayo mahubiri. Mnajua ni bora zaidi kuniishia moja kuliko kunihubiria moja, naamini, kwa sababu naweza—na—naweza kuyaona maisha yako. Mungu huyaangalia maisha yetu, na ulimwengu huyaangalia maisha yetu, anataka kujua maisha yetu ni nini.

¹⁸ Nao watu wanatujua, haidhuru, matendo ye—yetu yana sauti kubwa sana hata huuzamisha ushuhuda wetu. Inategemea kile tunachosema: Kama sisi ni Wakristo, wala hatuyaishi, basi watu wanajua vizuri zaidi; lakini wakati sisi ni Wakristo, na kusema sisi ni Wakristo, na kuishi kama Wakristo, maisha yetu

yatafanya hivyo hata tusiposema jambo lingine. Maisha yetu, sisi ni nyaraka zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote, kwa hiyo wanaangalia jinsi unavyoenenda.

¹⁹ Nami nilikuwa nikiwazia hivi majuzi kuhusu kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu, muhuri hutiwa alama pande zote mbili, wanakuona ukija, na kukuona ukienda. Ukija unaonekana kama Mkristo, ukiondoka unaonekana kama Mkristo, kwa hiyo, wakati umetiwa muhuri na Roho Mtakatifu.

²⁰ Kwa hiyo usiku wa leo ni—nina mhubiri pamoja nami, Ndugu Jack Moore, nina hakika ninyi nyote mnamfahamu. Na—nami kwa namna fulani nimeshuka kuja kuwaombea baadhi ya jamaa wagonjwa, naye Ndugu Jack alikuwa ahubiri kwa niaba yangu, kwa hiyo nina hakika mlifurahia ujumbe wake, yeye—yeye ni mnenaji mzuri.

²¹ Na—na mimi—mimi si mhubiri, kwa hiyo kwa namna fulani sikuzote nilisema nilikuwa tairi ya akiba; nayo tairi ya akiba, unaitumia wakati unapopata pancha. Sasa, hatuna pancha yoyote, mnaweza kuona hilo usiku wa leo, lakini *kwa namna fulani au nyingine* tutabingirika kidogo kwa tairi la akiba, labda, kama Bwana ataruhusu.

²² Sasa, nafikiri wana mahali pengine wanapoenda kesho usiku, nasema hivyo kwa ajili ya watu walio nje, ambapo, ninaamini, kutakuwa na nafasi ya kuketi. Hiyo ni kweli, Ndugu, Mchungaji? Lakini ninashukuru kwa ajili ya fursa ya kufikia jibu la maombi ya ndugu huyu.

²³ Mungu alibariki kanisa hili, ambariki ndugu huyu, kusanyiko lake lote, hili kundi zuri la wachungaji washirika. Mtu fulani aliniambia, ninasahau ni makanisa mangapi yalikuwa yakija kushirikiana kufanya mkutano. Bila shaka ninathamini hilo, ndugu. Sisi—sisi hatujagawanyika, sisi sote ni mwili mmoja.

²⁴ Hilo lilithibitika *sana* huko—huko Houston, wakati Malaika wa Bwana alipopigwa picha Yake kwa mara ya kwanza huko. Wakati kuna kitu fulani shirika, uponyaji wa Kiungu ulikuwa hatarini, kile sisi sote tunachoamini, ndipo tofauti zetu ndogondogo zikasahaulika, kila mtu akashiriki tu moja kwa moja, wakaja pamoja.

²⁵ Nafikiri...Wakati Sulemani alipojenga lile hekalu la kwanza yalikatwa kutoka kote ulimwenguni, yakatumwa kwa meli, yakakatwa kutoka machimboni, na—nayo mierezi ikakatwa huko Lebanoni, na kufanywa kuelea mpaka Yafa, kisha kuvutwa na mkokoteni wa maksai, na kadhalika. Nalo lilikuwa limejengwa kwa ustadi sana hata wakati hekalu lilipounganishwa, lilikuwa na kila namna ya mawe madogo ya kipekee ndani yake, lakini walipoanza kusoma ramani, yote yalikuwa kwenye ramani, na hapakuwapo hata na sauti ya

msumeno, wala sauti ya nyundo kwa muda wa miaka arobaini katika kulijenga hilo hekalu.

²⁶ Nafikiri hivyo ndivyo Mungu amewakatakata watu Wake kabisa, mmoja ana tabia ya namna moja, mwingine nyingine, bali wote ni Wakristo, mawe yaliyounganishwa, yaliyounganishwa pamoja juu ya Jiwe Kuu la Pembeni, Kristo Yesu. Loo, hilo hapo Jambo muhimu! Wengi sana wanalikataa Jiwe hilo la thamani la Pembeni, ambapo sote tumejengwa pamoja, tukaunganishwa pamoja kwa upendo wa Mungu, hiyo ni kweli, upendo wa Mungu. Na tunapokuwa na huo, hakuna kitu kitakachotutenganisha, hakuna kitu kinachoweza kutugawanya, maadamu tunapendana.

²⁷ Nimekuwa mhudumu kwa miaka thelathini na mmoja, nimeona karama za kila namna, nime—nimemwona Mungu akitenda mambo makuu, lakini jambo kuu kuliko yote nililopata kuona maishani mwangu lilikuwa ni upendo. Ndio uwezo wenye nguvu kuliko wote ambao huzuia chochote kilichopo, ni upendo, upendo uliomsukuma Mungu mwenye nguvu. “Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee.” Upendo ndio kiini kikuu, kitu tu—tunachoacha, ni kitu ambacho ni cha Milele.

²⁸ Nilikuwa nikizungumza leo, tukija pamoja na Ndugu Moore, nikasema, “Hebu chukua kama upendo wa, upendo, upendo wa kawaida, upendo wa kibinadamu, unaoitwa upendo wa *fileo*, Upendo wa kiungu ni *Agapao*, lakini katika upendo wa fileo, unatoka nje, unamwona Mariamu na Martha, unaambatana na Martha, tuseme, ki—kisha unamwona Mariamu, kuna kitu fulani kumhusu Mariamu ambacho ni tofauti na Martha, ingawa Martha ndiye mrembo zaidi, hata hivyo unampenda Mariamu zaidi.” Sasa, kama kuna Mariamu na Martha hapa, sininii... Ninatumia tu hilo kama... mwajua.

²⁹ “Kwa hiyo, lakini unaona ya kwamba ndiye msichana unayempenda, kuna jambo fulani kumhusu, mara unapomwona, unajua unampenda, unawazia, ‘Loo, jamani, laiti ningalipata tu miadi na msichana huyo!’ Vema, hatimaye unaipata, unafikiri ingeridhisha hisia hiyo, hairidhishi. Ndipo unawazia, ‘Kama ningeandelea kufanya urafiki naye, hilo lingetosha.’ Hatimaye, unaendelea kuwa naye taratibu, hairidhishi. ‘Kama angeniruhusu nimuage usiku kwa busu wakati mwingine, hilo lingeniridhisha.’ Lakini, hatimaye, hilo linatukia, wala haliridhishi. ‘Vema, kama ningemwoa, najua lingeridhisha.’ Haliridhishi.

³⁰ “Hata uhusiano wa kifamilia, unampenda sana, unajisikia kama ungeweza kumvuta kote kupitia kwako, na kunyosha mkono, na kumvuta tena, ukijaribu—ukijaribu kuninii... Huo ni usemi fidhuli, sikuumaanisha hivyo, mnaona. Lakini na—namaanisha, kile ninachojaribu kusema, *unampenda*, *unampenda*, *unampenda*, wala hakuna mahali unapoweza

kupata . . . Ni kitu gani? Yeye ni sehemu ya nafsi yako, yeye ni sehemu yako, hiyo ni kweli.”

³¹ Hiyo ni—hiyo ni . . . Na kama . . . Hivyo ndivyo Mungu alivyo. Unapokuja na kumwona Kristo moyoni mwako, hakuna mahali unapoweza kusimama, unazidi tu kusonga mbele, mkutano *huu*, mkutano *ule*, kitu *hiki*, kitu *kile*. Ni:

Upendo wa Mungu, jinsi ulivyo mwingi na safi!
Jinsi usivyopimika na wenye nguvu!
Utadumu milele,
Wimbo wa watakatifu na malaika.

Loo, mimi . . . Watu wakijaribu kuupima upendo wa Mungu, mmoja wao aliandika:

Kama tukiijaza bahari kwa wino,
Na mbingu zingalifanywa kwa karatasi za ngozi;
Kila shina duniani liwe ni unyoya wa kuandikia,
Na kila mtu awe ni mwandishi;
Kuandika upendo wa Mungu Juu
Kungeikausha bahari; (Jamani!)
Na gombo lingeweza kuenea wote,
Ingawa limetandazwa anga kwa anga.

³² Jinsi upendo wa Mungu ulivyo! Kwa hiyo hilo ndilo tunaloamini, kupendana.

³³ Yohana, baada ya kurudi kutoka kisiwa cha Patimo huko nje katika Bahari ya Aegea, jambo pekee aliloweza kusema lilikuwa, “Watoto wadogo, pendaneni.” Aliona kulikuwa na *kitu* halisi.

³⁴ Na huyo alikuwa ni yule mwanafunzi aliyetaka kuagiza Moto ushuke mjini na kuwateketeza, maana hawangempa Yeye chakula cha kutosha. Lakini jinsi Kristo alivyomshika, na kumjulisha, “Hujui una roho wa namna gani,” Yeye alisema. “Akijaribu kuuangamiza uhai, tunakuja kuokoa uhai.” Huo ndio tunaopaswa kuwa nao, ni upendo mmoja kwa mwingine.

³⁵ Katika huduma yangu tangu nilipowaona, nimekuwa karibu kote ulimwenguni, safari kadhaa nchi za ng’ambo, safari saba ama nane miongoni mwa makafiri, na kila mahali, nami ninaona jambo hili, ya kwamba kitu chenye nguvu sana ninachoweza kuwazia ni upendo. Kama ninamwombea mtu fulani, kama siwezi kuwa na hisia ya mtu huyo moyoni mwangu, kamwe haifai kitu.

³⁶ Wakati ninapoweza kuwazia pale, “Vipi kama ningekuwa nimesimama mahali pao, vipi kama huyo angekuwa ni mtoto wangu mchanga, vipi kama huyo angekuwa ni mama yangu, mke wangu, dada yangu, ndugu yangu?” unapojisikia hivyo kwa ajili yao, basi kitu fulani kinaanza kutokea, huruma inatoka na kumshika huyo mgonjwa, inawarudisha.

37 Sasa, marafiki, ninajua ya kwamba Mungu anawapenda. Na sasa, hatutaki kuchukua wakati mwingi sana, kwa sababu ninataka tu kusoma Andiko moja ama mawili, kisha kwa namna fulani tuzungumze kwa dakika moja au kitu kama hicho, kuninii, dakika chache, hasa, tupate kujua tu aina ya hisia ya Roho.

38 Sasa, kila mmoja wenu ni roho, mnajua hilo, wewe ni nyama, una mwili, lakini huo ni wako, *wewe* ni nani ndani yake? Unaona? Hiyo ni roho yako, hiyo ndiyo tunayopaswa kuishika, ni ile iliyo ndani. Tunaomba, na kumwuliza Mungu atusaidie.

39 Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja, tunapomwendea katika maombi. Wewe uliye nje, Bwana akubariki. Nikiangalia kupitia madirishani, nikiwaona watu wakiinamisha vichwa vyao huko nje, Wakristo waaminifu kwelikweli.

40 Bwana mwenye rehema, sasa tumekuja pamoja, na tuna furaha sana kwa sababu tunaweza, na kufanya ushirika sisi kwa sisi huku Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ikitusafisha na udhalimu wote. Ninawazia tu juu ya hatari nyingi, taabu, na mitego ambayo tumepitia tangu tulipokutana hapa awali, huku Beaumont, Texas. Ni wangapi, tungeweza kusimama usiku wa leo na kushuhudia, kila mmoja wetu, yale ambayo tumepitia tangu wakati huo, na kuwazia ya kwamba neema ya Mungu imetuleta salama umbali huu, tunaamini ataninii... Neema Yake imetosha kutuvusha.

41 Ninakushukuru kwa ajili ya kanisa hili, kwa ajili ya watu hawa, kwa ajili ya makanisa yanayoshirikiana, kwa ajili ya watoto Wako wote kote nchini, humu. Mungu, ninaamini Texas itawakilishwa sana Utukufuni, kwa ajili ya hawa wahudumu hodari, watumishi Wako ambao wamevuka jimbo hili, na wameleta Injili na watu kwa ajili ya Ufalme Wako. Ninakushukuru kwa ajili ya kila mmoja wao.

42 Mungu, ifunge mioyo yetu karibu sana pamoja na vifungo vya upendo, hata hakuna kitu kilichopo, cha usoni, ama kingeweza kuja, ambacho kingeweza kututenganisha na upendo wa Mungu ulio katika Kristo. Tujalie, Bwana.

43 Sasa, tunakukaribia Wewe kuomba rehema, usiku wa leo. Nadhani sehemu kubwa zaidi ya watu hawa katika kanisa hili, usiku wa leo, ni wafuasi hapa. Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utakuja katika nguvu kuu, na utamponya kila mgonjwa au mtu anayeteseka aliye katika Uwepo wa Kiungu. Tunatambua ya kwamba baraka hii ni baraka ambayo umempa mwaminio, uliiahidi, nasi tunaamini kila Neno lake kwamba ni kweli. Ninaomba ya kwamba Roho Mtakatifu mkuu, usiku wa leo, atawajalia baraka hizi, nasi tutakusifu kwa ajili yake, katika Jina la Bwana Yesu.

⁴⁴ Na, Baba, tunatumaini ya kwamba katika kuja huku, kumalizia kwa juma hili, na maadamu Wewe ungetaka tuwe hapa, jalia watu waokolewe, kwanza. Jalia wale wasio na ubatizo wa Roho Mtakatifu waingie, na kupata ushirika pamoja na Mungu, na kutembea katika Utukufu wa Shekina wa Uwepo Wake kwa ubatizo wa Roho.

⁴⁵ Tunaomba ya kwamba utawasaidia watumishi Wako, Bwana, wahudumu, ndugu zangu, watoto Wako. Jalia wavuviwe sana hata watachukua msimamo mpya, watoke mkutanoni wakiwa na azimio, Bwana Mungu, kuitepeka Injili mbali zaidi kuliko walivyopata kufanya bado. Wape watu kwa ajili ya ujira wao, miujiza mikuu na ishara na zikafuate huduma yao wapate kumwinua Bwana Yesu.

⁴⁶ Bariiki kila kanisa, jaga tele kila kanisa, Bwana, na jalia tushindilie vingi vyetu vya hema mbali nje ya mipaka sasa. Jalia tuvishindilie hata nje ya mipaka ya kimadhehebu, Bwana, ili tuweze kuvitupia viumbe vyote vya Mungu kote nchini mkono wetu wa upendo, tuwavute waingie katika ushirika wa Bwana Yesu. Tujalie, Bwana, nasi sote tutakusifu, kwa kuwa tunaomba baraka hizi, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Katika masomo ya Injili usiku wa leo, kwa muda mfupi tu sasa kabla hatujaanza, mstari wa maombi kuwaombea wagonjwa...

⁴⁷ Sasa, mwanangu, ama Bw. Goad hapa, ama Bw. Mercier, wenza wangu watatu katika huduma, ama labda Ndugu Moore, baadhi yao watakuwa kanisani kila jioni kugawa kadi za maombi, popote watakapofanya ibada ya usiku huo.

⁴⁸ Wengi wenu mnakumbuka jinsi tulivyolifanya mara ya mwisho, kugawa kadi za maombi, halafu mahali fulani, tunapoingia mle, vema, tunaanza kutoka kwenye namba fulani na kuita kundi la watu jukwaani. Na wakati mwingine hata hatugawi kadi za maombi na—na tunawaleta tu bila mpangilio, na, ama wakati mwingine Roho Mtakatifu huenda tu juu ya kusanyiko na kuwachukua, kwa vyovyote vile.

⁴⁹ Kwa hiyo siyo, kadi za maombi hazina uhusiano wowote na—na uponyaji wako, kadi ya maombi haina uhusiano wowote nao, ni imani yako katika Mungu. Kama Mungu akiendelea jinsi ambavyo amekuwa, mtaona ya kwamba katika usiku ujao ama hivyo, kwamba wakati mwingine ambapo mmoja hapa jukwaani anaponywa, kuna kuponywa hamsini huko nje kunakofanyika.

⁵⁰ Wala si kila mtu anayekuja jukwaani anayeponywa, Mungu huponya kulingana na imani yako, unaona, si kulingana na uanachama wako, si kulingana na haki yako. Nimemwona mtakatifu akipita na kukosa uponyaji wao, huku kahaba naye anafuata nyuma yake na kuponywa. Mnaona? Ni kulingana na imani yako, msingi wake ni juu ya imani yako, “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.”

⁵¹ Sasa, fungueni Yohana Mtakatifu, mlango wa 12, nasi tutasoma cha kwanza, uh, nitasoma vifungu viwili vya mlango wa 12 wa Yohana Mtakatifu, kifungu cha 20 na cha 21, si kuhubiri, bali kupata tu nukuu ndogo kwa ajili ya upako kuingia jengoni, na nje ya jengo, popote pale, ili Mungu apate kuwaponya watu usiku wa leo.

⁵² Sasa, ninawatakeni mweke nia yenu sawa juu ya jambo moja, juu ya Bwana Yesu. Sasa, kumbukeni, hakuna mtu aliye mponyaji, hilo ni kosa. Yote ambayo Mungu angeweza kutufanyia yalifanywa kwa ajili yetu pale Kalvari. Na hapo ndipo kila mpango, mpango wa wokovu, ambapo upatanisho kwa ajili ya uponyaji, na kwa ajili ya wokovu, ambapo kila sifa ya Uzima Wake inaweza kuonyeshwa kwetu, ilitimizwa pale Kalvari na kumalizika.

Unasema, “Ati wokovu? Ndugu Branham, mimi sikuokolewa pale Kalvari.”

Vema, kama hukuokolewa pale, kamwe hutaokolewa, hiyo ni kweli. Uliokolewa miaka elfu moja mia tisa iliyopita.

Unasema, “La, la, Ndugu, niliokoka juma lililopita.”

⁵³ La, uliukubali juma lililopita, bali gharama ililipwa, kwa kweli uliokolewa miaka elfu moja mia tisa iliyopita, uliponywa miaka elfu moja mia tisa iliyopita. Sasa, unataka kuukubali lini? Sasa? Vema. Huo ndio wakati wa kuukubali, sasa. Sasa, kazi imekwisha, kila kitu kimekwisha. Yote makam-. . . Yote tunayohitaji katika safari ya kutoka duniani hadi Utukufuni yamekamilika katika Kristo, na Kristo ndani yako.

⁵⁴ Wakati mti. . . Ninyi watu hapa Texas ni hodari wa tunda. Wakati mti mdogo umewekwa wenye ukubwa kama *huo*, tuseme mpichi mdogo. . . Sasa, mama yangu anatoka Paris, Texas, kwa hiyo mimi ni Mteksas kidogo tu, mwajua, kwa hiyo, vya kutosha kuipenda sana, na watu wake. Sasa, wakati mti mdogo. . . Alikuwa, nchi ya pichi.

⁵⁵ Mti mdogo usiozidi urefu wa nusu inchi, hivi mlijua kila pichi litakalowahi kuwa kwenye mti huo liko ndani yake wakati huo? Kama sivyo, linatoka wapi? Umpandwa ardhini, nao hauna budi kukua, na hauna budi kunywa. Nao unakunywa kutoka kwenye maji ya ardhini, na humo ndani unaingiza vitamini, na kadhalika, ukizileta kutoka ardhini unapokunywa, nao unakunywa zaidi ya sehemu yake uliyogawiwa, kwa hiyo kadiri unavyokunywa, ndivyo unavyozidi kusukuma nje. Unasukuma nje matawi, kisha unasukuma nje majani, kisha unasukuma nje maua, kisha unasukuma nje mapichi.

⁵⁶ Vema, hivyo ndivyo Mkristo alivyo. Tunapopandwa katika Kristo Yesu, ile Chemchemi ya Uzima isiyomalizika, kila kitu tunachohitaji kiko ndani yetu basi, tunaendelea tu kunywa na kusukuma nje, kunywa na kusukuma nje. Kama tuna haja zaidi

ya Mungu, endelea tu kunywa na kusukuma nje; kama tunahitaji uponyaji, kunywa tu na usukume nje. Hivyo tu. Ninii tu. . .

⁵⁷ Mungu alimwambia Yoshua, “Kila mguu wa nchi, popote ninii wako. . . Kila kipande cha ardhi ambacho mguu wako utakanyaga, ninakupa wewe kama milki yako.” Kwa hiyo alama za miguu zilimaanisha umilikaji. Naye Mungu ametupa kila baraka tunayohitaji na tutakayoomba, na jambo pekee tunalopaswa kufanya ni kuipokea. Sasa, Mungu hataileta na kukupa wewe, huna budi kwenda kuichukua, ni yako. Mnaelewa sasa kila mtu? Hatuna budi kuimiliki, ni yetu.

⁵⁸ Mungu alimwambia Musa huko chini Misri, “Nimewapa hiyo nchi,” bali ilikuwa imejaa Waamori, Wahiti, na namna zote mbalimbali za *waa* na *waninii*. Lakini Mungu angeliweza kwenda kule juu na kusababisha dhoruba ipitie kule, na kuwafagilia wote mbali, kasema, “Karibuni ndani, enyi watoto.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ? . . . hafanyi hivyo. Alisema, “Nimewapa, sasa nendeni mkaiteke.”

⁵⁹ Sasa, inategemea unaangalia nini. Kulikuwako na wengi wa wapelelezi walioenda kupeleleza, wakarudi, kumi kati yao, na kuleta taarifa mbaya, “Hatuwezi kufanya hivyo, ingetuharibu, wao ni wakubwa kuliko tulivyo sisi,” yote hayo. Lakini wawili walikuwa na ushahidi, wawili walirudi, kwa sababu inategemea kile walichokuwa wakiangalia. Hao wengine walikuwa wakiwaangalia Waamori, na Wahiti, na kadhalika, lakini Yoshua na Kalebu walikuwa wakiangalia ahadi ya Mungu, kwa hiyo wakasema, “Sisi tunaweza hata na zaidi kuiteka.”

⁶⁰ Sasa, unaangalia nini usiku wa leo? Angalia ahadi ya Mungu, na uendelee kunywa na kusukuma. Basi ukifanya hivyo, jambo fulani litatukia.

⁶¹ Kama sikuwazia ningekuwa baraka kwenu, hakika nisingekuja hapa, ni—nisingekuja. Nisingekuja, niwaambie jambo fulani la kuwadanganya, kwa sababu kama sikujua kwamba ni kweli, basi ningekaa nyumbani. Ningeshuka nije nikawapeni mikono, niwatembelee, niende nyumbani, nione ni nani aliyekuwa na mpishi bora kuliko wote, na—na halafu nije, nirudi nyumbani, niende kuvua samaki pamoja nanyi, ama *kitu kama hicho*, ama—ama kitu kama hicho. Lakini ninajua ya kwamba jambo ninalozungumzia, uponyaji wa Kiungu, wokovu, mambo hayo ni halisi, halisi kuliko tulivyoketi hapa.

⁶² Sasa, hebu na tuamini kwa moyo wetu wote tunaposoma. Yohana Mtakatifu, mlango wa 12, kifungu cha 20 na 21:

. . . palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda kuabudu kwenye sikukuu:

Basi hao walimwendea Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya, wakamwambia, wakisema, Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu.

⁶³ Na sasa, kama ningeliita hilo somo dogo, mazungumzo madogo, ninataka kuchukua Waebrania 13:8, hiyo imekuwa ndiyo mada yangu katika miaka hii yote: *Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele*.

⁶⁴ Sasa, hebu tujiulize tu swali hili. Watu hawa huja, nami ninaamini ya kwamba kila mmoja wetu usiku wa leo yuko tu kama walivyokuwa, walikuwa wamesikia habari za Yesu, kwa hiyo walitaka kumwona. Wala si—siamini kuna mtu yeyote angaliweza kusikia juu ya Utu huo wa kupendeza wa Bwana Yesu, ila ambaye shauku ya moyo wake wote ni kumwona Yeye. Niliposikia Jina hilo kwa mara ya kwanza, kuna *kitu fulani* tu, utamu sana Kwalo, ni—nilitaka kumwona.

⁶⁵ Vema basi, kama walikuwa wakitamani... Walikuwa ni wanadamu, kama mimi na wewe tulivyo. Nao walikuwa wamesikia habari Zake, nao wakaja kumwona, basi shauku yao ilikuwa ni kumwona, nao wakapata majaliwa ya kumwona.

⁶⁶ Sasa, kama Yesu Kristo ni, na Mungu anisamehe kwa kusema *kama*, simaanishi kukufuru, bali kutoa hoja, kama Yesu Kristo *ni* yeye yule jana, leo, na hata milele, nasi tuna shauku ile ile, basi kwa nini hatuwezi kumwona, kama Yeye angali ni yeye yule? Sasa, Yeye hana budi kuwa yeye yule kama Biblia inasema Yeye ni yeye yule.

⁶⁷ Yeye ni Mwokozi yeye yule, Mponyaji yeye yule, na vile vile tu alivyokuwa. Kitu pekee kilicho tofauti ndani Yake, Yeye sasa yuko katika mwili usioonekana, hapo ndipo alipokuwa katika mwili unaonekana. Lakini Yeye aliahidi ya kwamba, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi,” na *Mimi* ni kiwakilishi nafsi, “nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari,” ama wakati.

⁶⁸ Sasa, kama Yeye ni yeye yule, na aliahidi ya kwamba “Ninyi...Sasa, bado kitambo kidogo na ulimwengu,” hilo ni “kosmos,” ambalo linamaanisha *utaratibu wa ulimwengu*, “hautaniona tena, bali ninyi mtaniona,” hilo ni Kanisa, mwaminio, “kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari,” basi hilo linamfanya yeye yule jana, leo, na hata milele. Yohana Mtakatifu 14:12, Yeye alisema, “Yeye aniaminiye Mimi kazi nizifanyazo, yeye naye atazifanya.” Kwa hiyo tunaona Maandiko, hatuwezi kuyakana Maandiko hayo, Yapo.

⁶⁹ Sasa, kama hatuna imani ya kuyafanya yajibu, vema, hebu tuseme tu, “Ninayaamini, bali sina imani ya kufanya hivyo.” Hiyo ni kama tu, laiti ningalikuwa na imani kama aliyokuwa nayo Henoko. Siku moja alitembea na Mungu baada ya miaka mia tano, alikuwa na ushuhuda kwamba alimpendeza, naye akachoka tu kuweka miguu yake ardhini, akafanya matembezi mafupi ya alasiri, akaenda Nyumbani pamoja Naye. Laiti

ningaliweza kufanya hivyo, lakini kama sina imani ya kufanya hivyo, sitamzuia mtu aliye na imani ya kufanya jambo hilo, nitamshukuru Mungu kwa ajili ya imani hiyo inayoweza kufanya hivyo.

⁷⁰ Hivyo ndivyo inavyotupasa kuwazia, tunaona wengine wakiponywa, wengine wanaukosa. Ni kitu gani? Ni ukosefu tu wa imani, hivyo tu. Mungu ha—hawatendei watoto Wake mmoja, njia moja, na mmoja, *nyingine*, msingi wake ni juu ya imani, nasi hatuna budi kuliadini.

⁷¹ Sasa, kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, basi kama tungeweza kuuliza swali lilo hilo. . . Sasa, sisi hapa, wengi wenu ninyi watu ambao mmekuwa mkimtumikia Mungu, nilipokuwa mtoto mchanga wa kiume, mwenye dhambi, mlikuwa mkimtumikia Mungu, nami nafikiri ya kwamba tuna haki ya kuja na kumwuliza Mungu swali lilo hilo ambalo hawa Wayunani waliuliza, “Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu. Tunataka kumwona.”

⁷² Nami nashangaa hili usiku wa leo: “Je, hiyo ingekuwa ndiyo. . . ? Hivi hilo lingekuwa ndilo lile kundi hili la watoto wa Mungu hapa Beaumont, Texas, mngetaka ku—mngetaka kumwona Yeye? Hakika ningependa kumwona. Mimi. . .

⁷³ Je, inawezekana kwamba tunaweza kumwona? Unafikiri hivyo? Bila shaka. Tuna njia nyingi tungeweza kumwona kama mtu huyo si kipofu kiroho. Nilimwona alasiri ya leo wakati jua lilipokuwa linatua, ninamwona huko nje kwenye mawimbi yenye povu ya kilindi, ninamwona katika nyota ya asubuhi, katika nyota ya jioni, ninamsikia akipiga kelele katika tai anaposhuka kupitia mlimani, ninamsikia akilia katika mbwa mwitu, ninamsikia—ninamsikia akilia katika kulungu, akiguna katika paa, mbona, bila shaka, ninamsikia akilia katika mtoto mchanga.

⁷⁴ Unajua, Yeye wakati mmoja alikuwa Mtoto, Mwenyewe. Nena kuhusu ishara! Isaya 9, walipoomba ishara Mungu aliwapa ishara kuu, “Bikira atachukua mimba, na kuzaa Mtoto. Ataitwa Jina Lake Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa milele.”

⁷⁵ Lilipaswa kuwa ni la kushangaza, Yehova, Mtoto mchanga, Yehova Mungu, Mtoto mchanga akilia horini juu ya lundo la samadi ho—horini. Lilipaswa kuwa la kushangaza, Yehova, Mvulana tineja, akicheza; Yehova, akipigilia misumari kama Seremala. Loo, jamani! Na zaidi ya yote, Yehova akitundikwa msalabani kuwaokoa wenye dhambi, lingepaswa kuwa la kushangaza.

⁷⁶ Tungeweza kumwona, Yeye hajafa. Si muda mrefu uliopita nilikuwa nikimzungumzia, huko Mexico, Ndugu Jack alikuwa huko usiku huo. Yapata. . . sisi. . . Karibu watu elfu thelathini walikuwa wamekusanyika pamoja, nasi tulikuwa tukiomba,

naye Mungu alikuwa akifanya ishara na miujiza. Na kulikuwako na maskini mwanamke mmoja kule chini, alikuwa na mtoto mchanga, naye maskini mtoto huyo akafa saa tatu asubuhi hiyo, ilikuwa yapata saa tatu usiku huo, na mvua ilikuwa ikinyesha.

⁷⁷ Na—na kwa hiyo, Billy akanijia, akasema, “Baba, hakuna njia ya kumwondolea mwanamke huyo mstarini.” Kasema, “Kamwe huwezi kumzuia,” kasema, “a—amepata wazimu.”

⁷⁸ Nami nikasema, “Vema, nyote mligawa kadi za maombi?” Na jina la ndugu huyo, mimi, tulimwita tu *Mañana*, kwa sababu alikuwa mwenda pole sana, kwa hiyo alikuwa ndiye aliyegawa kadi za maombi.

⁷⁹ Kasema, “Lakini hana kadi ya maombi, wala hana nyingine yoyote.” Kisha kasema, “Amekuwa akisimama hapa, wala hakupata kadi ya maombi.” Kasema, “Tuna kundi la mabawabu, nao hata hawawezi kumwondoa mstarini.”

⁸⁰ Nikamwambia Ndugu Moore, “Shuka uende, ukamwombee mtoto huyo mchanga, mnaona,” nikamtuma Ndugu Moore huko chini. Na kwa hiyo, wakati Ndugu Moore alipoanza kushuka, niliangalia mbele yangu, nami nikamwona mtoto mchanga, mtoto mchanga wa Kimeksiko ameketi mbele yangu, akipiga tu makelele na kucheka. Nikasema, “Ngoja, labda afadhali nishuke chini.”

Na kwa hiyo, hiyo blanketi ndogo ilikuwa imelowa maji. Wakamleta, na mara alipokuja, akaanza kulia kwa sauti kuu, “Padre, padre!”

⁸¹ Nikasema, “Hebu kidogo, mama.” Asingeweza kuzungumza Kiingereza. Naye alikuwa amemfunika huyo mtoto kwa blanketi. Nikamwekea mikono huyo mtoto mchanga, nami nikasema, “Bwana Yesu, dakika chache tu zilizopita Wewe ulinionesha ono. Je, huyu ndiye yule mtoto mchanga uliyenionesha? Alikuwa amekufa tangu hapo, asubuhi ya leo, naye huyo hapo alikuwa ameketi, akicheka?” Ndipo nilipoanza kuomba, maskini jamaa huyo akaanza kurusha mateke na kupiga mayowe chini ya blanketi hiyo.

⁸² Nami nikasema, “Sasa, usiandike hayo mpaka utakapoenda na kumwacha daktari atie sahihi taarifa hiyo kwamba huyu mtoto alikufa asubuhi ya leo saa tatu.” Naye akafanya hivyo.

⁸³ Sasa, ni kitu gani? Mungu ni Uzima, Yeye ni Uzima, Uzima wa Milele kwa wale... Nikaita roho ya mtoto huyo aliyekufa irudi katika mwili wa jamaa huyo mdogo.

⁸⁴ Sasa, Mungu, kama Yeye ni mkuu sana... Hapa wakati fulani uliopita, huko juu mahali ninapoishi kwenye mto Ohio, kulikuwa na mvulana mdogo aliyekuwa akishuka mtoni, naye angeenda, akishirikiana na mzee mvuvi. Alikuwa akija kanisani mwangu, alikuwa na ndevu ndefu, nyeupe. Kulikuwa na mahali fulani juu tu juu yetu panapoitwa Kisiwa Maili Sita, tulikuwa

tukivua samaki huko juu, naye mzee mvuvi alikuwa na nyavu zake, na kadhalika, huko juu. Kwa hiyo, mvulana huyo mdogo angepanda mtoni pamoja naye kutandaza nyavu hizi.

⁸⁵ Na kwa hiyo, mvulana huyo mdogo akaenda kwenye shule ya Jumapili huko mjini. Basi akaenda asubuhi moja na kumwuliza mama yake, akasema, “Mama,” kasema, “Jumapili iliyopita,” kasema, “mwalimu wangu wa shule ya Jumapili alikuwa akisimulia jinsi Mungu alivyo mkuu. Kasema Yeye hufunika anga lote, kamwe hakuanza, na kadhalika.” Kasema, “Kama Yeye ni mkuu hivyo, kama Yeye ni mkuu hivyo, basi Yeye ni mkuu kuliko nilivyo mimi;” kisha kasema, “kama Yeye ni mkuu, mkuu hivyo, Yeye ni mkuu kuliko mlina; kama Yeye ni mkuu hivyo, Yeye ni mkuu kuliko mto,” kisha kasema, “Ninaweza kuona vitu hivyo vyote, kwa hiyo kwa nini siwezi kumwona Mungu, kama Yeye ni mkuu hivyo?” Hilo ni swali zuri sana.

Kwa hiyo akasema, “Sasa angalia, Mpenzi, mimi si mwalimu wa shule ya Jumapili, nenda kamwulize mwalimu wako wa shule ya Jumapili.”

Vema, akaenda kwa mwalimu wa shule ya Jumapili, akasema, “Siwezi kujibu hilo, nenda kwa mchungaji.”

Naye mchungaji akasema, “Mbona, la, mwanangu, hakuna mtu anayeweza kumwona Mungu.”

Kasema, “Vema, vipi...? Yeye akiwa ni mkuu hivyo, hatuwezi kumwona?”

Akasema, “La, hakuna mtu anayeweza kumwona.”

⁸⁶ Vema, kasema hakupendezwa na jibu hilo sana, lakini akaendelea, maana hicho kilikuwa ndicho kiwango cha juu zaidi angaliweza, alichowazia angeweza kwenda, kilikuwa ni mchungaji.

⁸⁷ Kwa hiyo, siku moja wakishuka mtoni pamoja na huyo mvuvi mzee, kukatokea dhoruba, naye mzee mvuvi akaingia ukingoni. Na kwa hiyo, baada ya dhoruba kwisha, ha—hao wawili wakaanza kuteremka mtoni pamoja. Na, loo, jinsi hewa, safi sana baada ya mvua!

⁸⁸ Na—nalo jua lilikuwa likishuka magharibi, ndipo kule mashariki ukaja upinde wa mvua. Naye mvulana huyo mdogo ameketi kwenye—kwenye shetri ya hiyo mashua, maskini mvuvi akivuta makasia, akaona machozi makubwa meupe mno maangavu yakitiririka kwenye ndevu zake zenye mvi. Ndipo mvulana huyo mdogo akaangalia kote kuona kile alichokuwa akiangalia, ilikuwa ni upinde wa mvua.

⁸⁹ Kwa hiyo yeye...walikuwa...Dini haikuwa imetajwa miongoni mwao kwa muda, kwa hiyo, akaenda mbele, katikati ya mashua, naye akamwambia, akasema, “Bwana, nitakuuliza swali ambalo mama yangu, mwalimu wa shule ya Jumapili, wala

mchungaji hawezi kuniridhisha.” Akasema, “Mungu aliumba ule upinde wa mvua, sivyo?”

Akasema, “Naam, bwana, aliuumba, mwanangu. Alitoa hiyo, ahadi ya kwamba hatauangamiza ulimwengu tena kwa maji.”

Akasema, “Kama Mungu ni mkuu sana, bwana, kama Yeye ni mkuu sana, basi kwa nini siwezi kumwona?”

⁹⁰ Maskini mvuvi huyo, akilemewa na swali la mvulana huyo mdogo, akavuta makasia kwenye mtumbwi, akamshika huyo mvulana mdogo, na kumkumbatia kifuani mwake, akamwinua juu, akamtazama usoni, akasema, “Mungu aubariki maskini moyo wako, kipenzi. Yote ambayo nimeona kwa miaka arobaini iliyopita imekuwa ni Mungu.”

⁹¹ Alikuwa na Mungu mwingi sana ndani, angeweza kumwona nje. Sasa, hivyo ndivyo inavyokupasa kumwona Mungu, ni kumwingiza ndani, na kumwacha aangalie kupitia macho yako. Lakini, mwajua, kanisa ni karibia limeingia katika hali ya kupooza, yanakuwa ya kawaida sana, mambo haya.

⁹² Hapa wakati fulani uliopita kulikuwako na mama mmoja huko Louisville, Kentucky, naamini ilikuwa, naye alikuwa na mvulana mdogo, akitembea kwenye duka la mali rahisi akitikisatikisa vitu vidogo, naye, akijaribu kumwonyesha, huyo mvulana mdogo aliketi tu amekodoa macho.

⁹³ Kwa hiyo yeye...Kila...Watu wakaanza kumtazama, akashikwa na mpagao, naye angesema, “Angalia, Mpenzi, angalia!” Naye mvulana huyo mdogo akakodoa tu macho. Kwa hiyo angeenda kwenye kaunta nyingine, na kuchukua kitu kinachopaswa kumvutia mvulana mdogo wa umri wake, na kusema, “Angalia, Mpenzi!” Naye angekodoa macho tu. Na kwa hiyo, hatimaye, ikawa amelemewa kabisa, na kudhoofika, mpaka akaanguka tu juu ya kaunta na kuanza kupiga mayowe, “La, la, la!”

Ndipo watu waliokuwa dukani wakamwendea na kusema, “Kuna nini, mama?”

⁹⁴ Akasema, “Mvulana wangu mdogo,” akasema, “jambo fulani lilimpata.” Akasema, “Si muda mrefu uliopita alikuwa maskini jamaa mchangamfu, lakini jambo fulani likampata, naye anaketi tu na kukodolea macho angani.” Kasema, “Hakuna kitu kinachopaswa kumvutia mvulana mdogo wa umri wake kitakachomvutia, yeye anakodoa macho tu.” Kasema, “Nilimpeleka kwa daktari, naye daktari akasema alikuwa mzima, lakini,” kasema, “sivyo, kwa sababu hataangalia chochote mtoto wa umri wake anachopaswa kuangalia.” Kisha kasema, “Yeye anakodolea tu macho angani.”

⁹⁵ Vema, hiyo ndiyo karibu hali ambayo makanisa yanaingia. Mambo hayo, Mungu ametikisa kila namna ya mwujiza na ishara

mbele ya kanisa, na bado wameketi, wakikodolea macho angani, kana kwamba tu hawakujua. . . Mungu katika nguvu Zake kuu katika miaka hii michache iliyopita amelitikisa Taifa hili kuliko hapo awali.

“Ati amelitikisa taifa?” Unasema, “Taifa la Marekani?”

⁹⁶ Taifa, Taifa Lake, Ufalme Wake. Mungu haahidi kutikisa taifa namna hiyo, Yeye anaahidi kulitikisa Kanisa Lake. Si Ujumbe wa kulitikisa taifa, ni Ujumbe wa kulitikisa Kanisa. Anakuja Kanisani Mwake kuwaamsha, taifa halitaamini, hata hivyo, *huko* nje.

⁹⁷ Yesu kamwe hakuliendea taifa, “Alienda kwa walio Wake, walio Wake hawakumpokea.” Hakuja kamwe kwa ulimwengu. Maelfu na maelfu kamwe hawakujua hata alikuwa Palestina wakati wa ziara Yake, bali inatumwa kwa Kanisa.

Sasa, kama ningewaambia ninyi ndugu wa Kimethodisti, “Je, Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele?”

⁹⁸ Mngesema, “Naam, tunaye katika kanisa la Kimethodisti, tunajua ndivyo alivyo.” Wabaptisti wangesema jambo lile lile, kila kanisa lingesema jambo lile lile.

⁹⁹ Tuna yapata, karibu madhehebu mia sita ama mia nane mbalimbali, kwa hiyo mtu fulani hana budi kuwa sahihi, na mtu fulani amekosea, kamwe haiwezekani kila mtu kuwa sahihi, ama kila mtu kukosea, hapana budi pawe na kweli na uongo hapo, mahali fulani.

¹⁰⁰ Kwa hiyo sasa, kama ningeliendea katika msimamo wa Kibaptisti, ama katika msimamo wa Kimethodisti, ama msimamo wa Kipentekoste, ama vyovyote nilivyoliendea, lingekuwa ni kuwadharau hao ndugu wengine. Hiyo ni kweli. Lakini sasa hebu na tuliendee kwa ukweli, hebu tuliendee kwa msimamo wa Biblia: Hebu na tuone kile alichokuwa jana, na kama tunaweza kuona kile alichokuwa jana, basi atakuwa ni yeye yule leo. Bila kujali theolojia yetu, wanasema Yeye alikuwa ni yeye yule. Sasa, vema, kama tunaweza kujua kile alichokuwa jana, basi tungeona kile alichokuwa leo.

¹⁰¹ Sasa, kama ningeweza kutoka na kumchukua mtu, na kuweka makovu ya misumari mikononi mwake, na—na alama za miiba kwenye paji la uso wake, hiyo ingekuwa. . . hiyo ingeweza kudanganywa, kwa sababu mtu huyo angeweza kuwa ni laghai, angeweza kuwa anamwiga Yesu Kristo. Njia pekee tutakayopata kujua Yeye alikuwa ni nini, ilikuwa ni kuona Maisha Yake yakitenda kazi katika Kanisa Lake. Kuacha Maisha Yake!

¹⁰² Kama—kama tawi la boga likizaa boga, kuna uhai wa boga kwenye tawi la mboga, huwezi kutoa matango kutoka kwake, kwa sababu ni mboga; kama ni tikitimaji, tikitimaji ndilo linalotoka kwenye tawi la tikitimaji; kama ni tawi la Kikristo, litamshuhudia Kristo. Kwa hiyo hebu tuone kile alichokuwa

jana, ndipo tutaona kile alicholeo, na kile atakachokuwa milele, nafikiri hilo linatupa sisi sote mtazamo mzuri.

¹⁰³ Hebu na turudi sasa katika Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza, tuone kile alichokuwa. Tunasoma katika Yohana Mtakatifu, nasi tungeweza kurudi hapa kwenye m—mlango wa kwanza wa Yohana Mtakatifu, nasi tungsoma hili. Sasa, hebu na tuanzie mwanzoni mwa maisha Yake na tuchukue vifungu vichache hapa, na halafu muda si muda mwajua, kesho usiku tutachukua mengine zaidi, na kuendelea tu kutafuta kujua kile alicholeo tunapoendelea.

¹⁰⁴ Lakini kwa kuwa hatuna ila kama dakika kumi na mbili, kumi na nne zaidi kabla hatujaanza mstari wa maombi, hebu tuwazie kile alichokuwa jana. Sasa, tunamwona hapa katika Yohana Mtakatifu, kama Injili zingine zote zinavyoanza, tunamwona katika—katika kuzaliwa Kwake, nasi tunajua jinsi huko kulivyokuwa kwa ajabu, ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, Uzao hasa wa mwanamke aliyeahidiwa katika bustani ya Edeni. Halafu basi tunaona ya kwamba kwenye umri wa miaka thelathini Yeye alibatizwa katika mto Yordani na Yohana Mbatizaji.

¹⁰⁵ Na wakati alipobatizwa, akitoka mara moja majini, tunaona ya kwamba Roho Mtakatifu, Mungu, kama katika mfano wa hua akitoka Mbinguni, na Sauti, ikisema, “Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa kukaa ndani Yake.” Na tafsiri sahihi ya hilo, “Ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake,” kwa sababu Mungu alikuwa ndani ya Kristo.

¹⁰⁶ Na sasa, aliposhuka juu Yake, Yeye akawa Mtiwa Mafuta, Masihi. Tunaona basi majaribu, akaingia nyikani, na mara aliporudi kutoka kwenye majaribu Yake akaenda huku na huku akiwaponya wagonjwa, akitoa pepo, akiwaweka watu huru. Hebu tuone basi, jambo la kwanza alilofanya lilikuwa ni kuanza kuhubiri Injili na kuwaponya wagonjwa, wale wote waliokandamizwa na ibilisi.

¹⁰⁷ Sasa, hebu na tuchukue baadhi ya ishara Zake. Sasa, je, Yeye ni Masihi? Sasa, tunatambua ya kwamba wamekuwa na uponyaji wa Kiungu hata kabla ya Yeye kuja duniani. Ni wangapi wanaojua hilo? Lile birika la Bethesda lilikuwa ni ishara ya uponyaji, na kote katika nyakati wamekuwa na uponyaji wa kila namna. Mnaona? Lakini kulipaswa kuwe na ishara ikimfuata huyu Masihi, Yeye alikuwa na ishara ya Masihi. Na kama Yeye alikuwa ni Masihi, ambaye ni Mtiwa Mafuta, Kristo, basi kulipaswa kuwe na ishara ya Masihi ikimfuata Masihi.

¹⁰⁸ Kuna ishara inayomfuata mwaminio. Mnaamini hilo? Mungu ni Mungu wa ishara, maajabu, na miujiza; na kama Yeye alikuwa hivyo mara ya kwanza, ndivyo alivyo mara ya pili, ndivyo alivyo mara ya tatu, ndivyo alivyo kila wakati.

¹⁰⁹ Kumbuka, unaposoma Neno la Mungu, kama vile sisi Waprotestanti tunavyoliamini kuwa ni Neno la Mungu lisiloweza kukosea, basi wakati Mungu anapoitwa jukwaani kutenda kazi, na inambidi kufanya uamuzi, jinsi Mungu anavyotenda juu ya kisa hicho hana budi kushughulikia kila kisa baadaye vile vile, kwa sababu ningeweza kufanya uamuzi leo, na unaweza kuwa sahihi, kesho huenda nikafanya uamuzi ule ule, ungekuwa ni mbaya, kwa sababu mwanzoni ulikuwa ni kosa, labda, lakini Mungu anapofanya uamuzi, ni mkamilifu, kwa sababu sisi tuna kikomo, sisi hukosea, Mungu hakosei, wala hana kikomo, wala hawezi kukosea. Kwa hiyo yale aliyosema Mungu ni kweli kabisa.

¹¹⁰ Na kama aliwahi kuitwa jukwaani kumwokoia mwenye dhambi, mtazamo aliochukua kwa huyo mwenye dhambi, itambidi kuwa na msimamo uo huo kwa kila mwenye dhambi mwenye kutubu tangu hapo. Kama aliitwa jukwaani kumponya mgonjwa, mtazamo aliochukua kwa mtu huyo mgonjwa, kila mgonjwa akija Kwake, hana budi kutenda vivyo hivyo, la sivyo alifanya makosa wakati alipotenda mara ya kwanza. Huyo hapo Mungu. Hiyo ni kweli?

¹¹¹ Kwa hiyo kile Yesu alichokuwa jana, hana budi kuwa yeye yule leo, la sivyo alikosea jana. Ishara Yake ya Masihi aliyowaonyesha watu wakati huo, kama hiyo ilikuwa ni kosa, basi ingembidi Yeye—Yeye kusema jambo lile lile leo. Na kama si... Halina budi kuwa sahihi, kwa sababu Yeye alikuwa ni Mungu. Na sasa, kama alikuwa sahihi wakati huo, na hiyo ilikuwa ni ishara, ni ishara ile ile leo, na itakuwa milele.

¹¹² Sasa, tutachukua baadhi ya matendo Yake. Mara baada ya Yeye kuanza kuhubiri kulikuwako na Andrea, mwajua, na hao walioanza kumfuata, wakamwuliza mahali alipoishi, baada ya kumwona Yordani siku hiyo, alipobatizwa na Yohana. Ndipo Andrea akaenda akamwona ndugu yake Simoni, kisha akamleta Simoni Kwake, “Njoo uone sasa, tumemwona Masihi.”

¹¹³ Simoni alikuwa mvuvi. Basi alipokuja katika Uwepo wa Bwana Yesu, akisimama pale, ni jambo gani la kwanza alilofanya Yesu? Hapana shaka alimtazama moja kwa moja usoni, na kusema, “Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona.”

¹¹⁴ Petro alikuwa amefundishwa, Simoni, hasa... Yeye aliitwa Kefa baada ya hapo, ambalo ni, tafsiri, “jiwe.” Alikuwa nini? Aliamini hilo, kwa sababu alikuwa na baba aliyekuwa amemfundisha, ya kwamba wakati Masihi atakapokuja, Myahudi halisi, wa kweli aliamini ya kwamba Masihi atakapokuja, Yeye angekuwa ni Nabii.

¹¹⁵ Myahudi daima waliwaamini manabii wao. Tunajua hilo, maana Musa alisema, “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi.” Yeye alikuwa Mungu-Nabii, Bwana Nabii, Mungu wa manabii. Lakini ishara Yake ilikuwa awe

ni nabii, nao walikuwa wakimtaalamia Nabii huyo. Hivi hamkumbuki, wao walisema, “Wewe ndiwe yule Nabii? Wewe ndiwe yule Nabii?” Walimwuliza Yohana, “Wewe ndiwe yule Nabii aliyekuwa aje?”

Akasema, “Watu husema mimi ni nani?”

“Wengine wanasema Wewe ni Eliya, ama Musa, na wengine, yule Nabii aliyekuwa aje.”

¹¹⁶ Walijua ya kwamba Yeye alikuwa awe nabii. Na wakati Simoni Petro, wakati alipomwambia, “Jina lako ni Simoni, na jina la baba yako ni Yona,” alijua upesi sana huyo alikuwa ndiye Nabii aliyekuwa ametabiriwa kuja, hiyo ilikuwa ishara ya Masihi kwake, ingawa hakuwa na elimu ya kutosha kuandika jina lake mwenyewe, bali alianguka miguuni pa Yesu, na akapewa funguo za Ufalme baadaye, kwa sababu alimpokea Mungu. Alijua kile kilichopaswa kumfuata. Alijua ya kwamba huyo alikuwa ni Mungu, ishara ya nabii.

¹¹⁷ Halafu kulikuwa na mmoja aliyesimama karibu, jina lake Filipo, tukija moja kwa moja kwenye mlango wa kwanza wa Yohana Mtakatifu, naye Filipo akafikiri hili lilikuwa ni la ajabu, na alipoona hili, aliridhika kwamba huyo alikuwa ndiye Nabii aliyenenwa habari zake, Masihi.

¹¹⁸ Kwa hiyo, kama huyo alikuwa ni Masihi jana, na ishara ya Masihi jana, itakuwa ni ishara ya Masihi leo kama Yeye ni Masihi yeye yule. Kweli, Yeye angekuwa ni kitu kile kile, hivyo ndivyo alivyowatangazia ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi.

¹¹⁹ Sasa, Filipo alikuwa na rafiki mzuri jina lake Nathanaeli. Uliwahi kuwa Palestina kuona mahali hapo palipokuwa? Yapata maili kumi na tano kuuzunguka mlima. Akakimbia kule, na jina la rafiki huyu lilikuwa ni Nathanaeli. Kwa hiyo, anapoenda kule kumtafuta Nathanaeli kumwambia habari hizi njema...

¹²⁰ Kuna jambo fulani kulihusu, kama ukiwahi kushawishika ya kwamba Yesu ndiye Kristo, huwezi kunyamaza, inakubidi tu kumwambia kila mtu kulihusu, hiyo ni kweli. Kamwe siwezi kuona jinsi watu wanavyoweza kupata upendo huu wa ajabu wa Mungu, na kunyamaza kimya nao. Loo, jamani!

¹²¹ Nilimwuliza mtu fulani si muda mrefu uliopita ambaye alisema walikuwa ni Mkristo kwa miaka *kadhaa*, nikasema, “Je, jirani zako wanajua hilo?”

Kasema, “La, kwa namna fulani hatulitangazi.”

Loo, jamani! Huwezi kufanya hivyo. Loo! Dada mmoja kanisani mwetu alikuwa akisimama na kuimba wimbo, “Ninakimbia, kukimbia, kukimbia, nami ninataka kulitangaza!”

¹²² Vema, hiyo karibu ni sawa, inakubidi tu kumwambia mtu fulani, huwezi kusimama kimya, *jambo fulani* limetukia, nawe unajua limetukia.

¹²³ Kwa hiyo alishawishika ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi. Hebu na tuchukue mchezo mdogo wa kuigiza kwa muda kidogo. Ninaweza kumwona Nathanaeli akizunguka, yapata safari ya siku moja, kuizunguka milima, juu ya mango, na hatimaye akaja kwenye nyumba ambamo Nathanaeli aliishi. Akabisha mlangoni. Na kwa hiyo, Bibi Nathanaeli akaja mlangoni. Akasema, “Mbona, Filipo! Mbona, ninafurahi kukuona!”

Kasema, “Yuko wapi Nathanaeli?”

¹²⁴ “Vema, Filipo, ndiyo kwanza aende kutembea bustanini mwa—mwake huko nje, yeye—yeye yuko huko nyuma mahali fulani. Utamwona, anaangalia kwenye ki—kijibustani chake cha mizeituni kule nyuma, ama, mitini, na kadhalika. Yuko huko nyuma kichakani, mahali fulani, utampata.”

¹²⁵ Nami ninaweza kumwona Nathanaeli akishuka kupitia kule, Filipo, hasa, akijaribu kumtafuta. Na baada ya kitambo kidogo, alikuwa amepiga magoti akiomba, hapo ni mahali pazuri kuwa. Kwa hiyo, na kwa kawaida hapo ndipo unapompata Kristo, unapokuwa umepiga magoti, hiyo ni njia nzuri, unaona. Kaa magotini mwako sana, ni vizuri. Basi alipokuwa chini ya mti huu akiomba, ninaweza kuwazia, bila shaka, Filipo, mwungwana Mkristo, mbona, alisimama tu na kungoja mpaka akamaliza kuomba.

¹²⁶ Ninaweza kumwona Nathanaeli akisimama, na kupangusa mavumbi magotini mwake namna *hiyo*, akisema, “Loo, Bwana abarikiwe, kwamba . . . Ninakushukuru, Bwana.” Akageuka, na kusema, “Filipo!”

¹²⁷ Sasa, yeye hakusema, “Bustani yote ikoje?” Mnaona? Ama, “Jamaa wote hawajambo? Na Yohana, Joe, na hao wote hawajambo?” mnajua. Hakusema hivyo. Alisema, “Njoo, mwone Yule tuliye mwona!” Loo, alikuwa tu akibubujika, ilimbidi kusema jambo fulani kulihusu. Ninapenda hilo.

¹²⁸ Loo, ninaamini Roho Mtakatifu kweli hujaza mpaka anabubujika. Daudi alisema kikombe chake kinafurika. Wengine, Roho Mtakatifu anapokushika, unabubujika tu.

¹²⁹ Hakuwa na wakati wa kuzungumza juu ya hilo shamba, alisema, “Njoo, mwone Yule tuliye mwona, Masihi! Tumemwona Masihi, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu. Njoo, uone Yule tuliye mwona, huyu ndiye yule Nabii aliyenenwa habari zake.”

¹³⁰ Ninaweza kuwazia huyu mwaminio mheshimiwa wa Kiothodoksi alisema, “Sasa, ngoja kidogo tu, Filipo, na—najua wewe ni mtu mzuri, mtu mzuri. Umeingia kwenye vurumai za namna gani? Umetumbukia kwenye wendawazimu gani? Sasa, una kasoro, mahali fulani. Daima nimekujua kuwa mtu mzuri, mwenye akili timamu, basi kwa nini unakuja hapa na kitu kama hicho, kwamba umemwona mtu, Yesu wa Nazareti, ulisema, ati mji wa Nazareti?”

¹³¹ “Vema, sasa, tunajua Masihi yuaja. Halafu basi, kama Masihi angekuja, unajua kile kingetukia? Ushoroba wa Mbinguni ungefunguka, Naye angeshuka moja kwa moja amwendee kiongozi wa dhehebu letu. Naam, bwana. Angeendesha moja kwa moja kwenye a—anga za hekalu. Na kama hakuja kwenye dhehebu letu, huyo si Yeye. Sasa, huyo si Yeye, Yeye hana budi kuja kwetu.”

¹³² Mnajua, hao kina Nathanaeli wote hawajakwisha bado. Kwa hiyo, “Hana budi tu kuja kwenye kundi letu, la sivyo Yeye haji kabisa.” Lakini mnajua, Mungu hufanya mambo jinsi anavyotaka Yeye, na...?...ni njia Yake.

Kwa hiyo, tunamwona akisema, “Sasa, je, neno lolote jema laweza kutoka Nazareti?”

¹³³ Nami nafikiri Filipo alimpa jibu zuri sana ambalo mtu yeyote angeweza, kasema, “Njoo, uone. Njoo uone. Usikae nyumbani na kukosoa, njoo, ujionee mwenyewe.” Hilo ndilo lililo bora kuliko yote.

“Loo, ninii yetu...Yeye kamwe...Si...Madhehebu yetu hayaudhamini, hatuko katika...hatushirikiani nalo, kwa hiyo nitakaa tu nyumbani, na...”

Vema kamwe hutajua basi. Hivyo tu. Unaona? “Njoo, uone.”

“Yachunguzeni Maandiko,” Yesu alisema, “Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi.” Mnaona? Tafuta kujua kama ni kweli ama si kweli.

Kwa hiyo, akasema, “Njoo, uone.”

¹³⁴ Sasa, ninaweza kuwazia, hebu na tuyaingilie mazungumzo yao wanapoendelea kando ya barabara, ninaweza kumsikia Filipo akimwambia Nathanaeli, “Nathanaeli, nawe huwezi kuamini hilo?”

“La.”

“Vema, hivi Maandiko hayasemi ya kwamba Bwana Mungu wetu atatuondokeshea Nabii kama—kama Musa?”

“Hiyo...Naam.”

“Vema, je, Masihi atakuwa ni nabii?”

“Naam, Yeye atakuwa ni nabii.”

“Je, ataonyesha ishara ya nabii?”

“Naam, Yeye ataonyesha ishara ya nabii.”

“Na hiyo itakuwa ndiyo ishara ya Masihi?”

“Naam, itakuwa.”

¹³⁵ “Vema. Sasa, je, unamjua maskini yule mvuvi asiye na elimu kule chini tuliyenunua wale samaki kutoka kwake siku ile, hakuwa na elimu ya kutosha kukutilia sahihi risiti?”

“Naam, naam, ninamkumbuka huyo. Loo, naam, ndugu yake Andrea, Simoni.”

“Naam, huyo alikuwa ndiye, maskini jamaa mkubwa, mnene, mwenye upara, amevaa aproni yenye gris.”

“Naam, huyo alikuwa ndiye.”

“Asingeweza kutia sahihi risiti?”

“Naam, hiyo ni kweli.”

“Vema, unajua, alikuja mbele ya Huyu tunayejua kuwa ndiye Masihi. Unakumbuka jina la baba yake lilikuwa nani?”

“Loo, hakika, nilikuwa na ushirika pamoja naye, Yona. Naam, ninamjua, Yona.”

“Vema, mara alipoenda mbele ya mtu huyu, alimwangalia, na kusema, “Jina lako ni Simoni, mwana wa Yona. Sasa, vipi kuhusu hilo?”

Filipo akasema, “Aa!” Ninamaanisha, Nathanaeli, “Aa!”

Filipo akasema, “Haitanishangaza kama Yeye asingekwambia *wewe* ni nani, utakapokuja kule.”

“Aa, sasa ngoja, si—sijui kuhusu hilo. Huh-um, la.”

¹³⁶ Baada ya kitambo kidogo wakawasili. Na labda Yesu alikuwa amesimama kwenye mstari wa maombi, ama—ama labda walikuja kwenye mstari wa maombi, sijui, lakini labda wao, alikuwa huko nyuma kwenye kusanyiko, popote pale, wakati alipokuja mbele za Bwana Yesu, Yesu aligeuka na kumwangalia, na kusema, “Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!” Hilo lilimduwaza.

¹³⁷ Sasa, unasema, “Loo, hakika, jinsi alivyokuwa amevalia.”

La, la, watu wote wa mashariki wanavalia vile vile. Walivaa hayo majoho, na vilemba, na kadhalika, jamii nyeusi ya watu.

¹³⁸ Kasema, “Aa,” kasema, “tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!” Kama ningelilisema, mtu mwema, mwaminifu, mtu mzuri, wa kidini, mwaminifu, Mwisraeli.

¹³⁹ Nalo likamduwaza, likamchoma kidogo, akasema, “Rabi,” maana yake ni *mwalimu*, “mbona, ulipata kunijua lini Wewe? Mbona, Wewe hujui lolote kunihusu mimi, sijawahi kukuona Wewe maishani mwangu, wala Wewe hujawahi kuniona maishani Mwako. Unajua kwamba mimi ni Mwisraeli, na mtu mwaminifu?”

¹⁴⁰ Sikilizeni, Yeye alisema, “Kabla Filippo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Macho ya jinsi gani, macho ya jinsi gani! Mauti hayawezi kuyafifisha, yako hai milele. “Nilikuona,” maili kumi na tano kuuzunguka huo mlima, siku moja kabla, “nilikuona.”

141 Jibu lake lilikuwa nini? “Rabi, Wewe ni Mfalme wa Israeli; Wewe ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli.” Kamwe hakuwa na swali lolote. Jina lake ni lisilopatikana na mauti usiku wa leo miongoni mwa wanadamu. Akaanguka miguuni Pake, “Rabi, Mwalimu, Wewe si mwanadamu tu, Wewe ni Mfalme wa Israeli. Wewe ni Mwana wa Mungu. Tunajua ya kwamba Masihi alikuwa afanye hivyo.”

142 Hapo walisimama wengine ambao hawakuamini hilo, mwajua. Walikuwa wameweka mikono yao nyuma yao, iliwabidi kulijibu kusanyiko lao, kwa sababu kusanyiko lilikuwa linaenda kuwaletea swali kuhusu jambo hilo. Wakasema, “Uh, *ahem!* Uh, bila shaka mtu huyu hufanya hivi tu kwa Beelzebuli, yeye ni mpiga ramli.” Mnaona? “Yeye hufanya hivi kwa Beelzebuli.”

143 Yesu akasema, “Ninawasamehe hilo, lakini saa yaja ambapo Roho Mtakatifu atakuja, Naye atafanya jambo lilo hilo, na neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe, si katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao.” Kwa hiyo mnaona mahali tunaposimama.

144 Kasema, “Nitakusamehe, ukinena hayo dhidi Yangu, nitakusamehe,” kwa sababu walimwita, walisema, Roho wa Mungu pepo mchafu, wakimwainisha Roho wa Mungu, akipambanua roho, huku Nabii, Mungu wa Milele, amesimama pale, akijitambulisha Mwenyewe katika ishara iliyoahidiwa kwamba angefanya, hayo Maandiko yakitimizwa machoni pao wenyewe, nao wamefungwa sana na madhehebu mpaka wao: “Vema, Yeye hakuja kwetu, kwa hiyo ni ibilisi.” Mnaona? Mnaona? Kweli tungeweza kwenda mjini kwa jambo hilo kwa muda kidogo, huko ni kwa watu *hawa*.

145 Lakini angalieni, hivyo ndivyo ilivyokuwa. Walisema ya kwamba Roho Mtakatifu angekuja siku moja, na kufanya jambo lile lile. Sasa, hivyo ndivyo...

146 Kumbukeni, kuna makabila matatu tu ya watu duniani, kama tunaamini Biblia, Watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, hao ni Wayahudi, Wamataifa, na Wasamaria. Mnamkumbuka Petro akiwa na zile funguo kwenye Siku ya Pentekoste? Halafu moja kwa moja hadi kwa Wasamaria, na hata kwa Mataifa, na hilo lililimalizia hilo, Wayahudi, Mataifa, Wasamaria.

147 Sasa, sisi Wamataifa, Waanglo-Sakson, hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote. Yeye huja tu kwa wale wanaomtazamia. Loo, ningetaka hilo likolee sana! Natumaini hilo linasimama juu kama miti hapa chini mbele yenu. Hilo, huwezi kuangalia bila kuliona. Yeye huja tu kwa wale wanaomtazamia. Sisi Mataifa hatukuwa tukimtazamia yeyote, hatukuwa tukimtazamia Masihi, bali Wayahudi na Wasamaria walikuwa wakimtazamia. Vema, tunaona jinsi alivyojitambulisha Mwenyewe.

148 Loo, sehemu zingine nyingi tungeweza kuwapeleka huko chini, bali hebu tufungue ukurasa mwingine. Tunaona basi ambapo alipitia kwenye bi—birika la Bethesda.

149 Na siku chache kabla ya hapo maskini mwanamke mmoja, alijaribu kuingia kwenye mstari wa maombi, hakuwa na kadi ya maombi, nadhani, na kwa hiyo, aliamini ya kwamba kama angeweza kumgusa Yeye, kwamba angeponywa. Na kwa hiyo, asingeweza kumwendea, huku watu wote wamemzunguka, na muda si muda mwajua, mbona, akapenya kisiri na kugusa upindo wa vazi Lake. Ndipo akasimama, na kusema, “Ni nani aliyenigusa? Mtu fulani amenigusa.”

150 Petro akamkemea. Naye akasema, “Lakini na—naona kwamba nimekuwa dhaifu, nguvu zimenitoka.” Aliangalia huku na huku juu ya kusanyiko mpaka akampata, na kumwambia kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma, kwa sababu *imani* yake ilikuwa imemwoko. Sasa, Yeye kamwe hakufanya hivyo, *imani* yake katika Yeye ilifanya hivyo. Loo, mnaliona? Imani yake! “Imani yako imekuoka.”

151 Sasa, ninataka watu hapa walio na ufasaha zaidi kuhusu hili, Ndugu Moore, na wengi wa hawa wahudumu wengine. . . Neno lilo hilo hapo ni *Sozo*, ambalo linamaanisha “kuokolewa,” kwa mwili au nafsi, vivyo hivyo tu, kuokolewa kimwili ama kuokolewa kiroho, vile vile unavyolifanya. Mwanamke huyo alimgusa.

152 Sasa, unasema, “Lakini Ndugu Branham, ninajua kile Yeye. . . Yeye alimgusa, sijui kama ningeweza.”

153 Biblia inasema ya kwamba Yeye, sasa hivi, ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli? Vema, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, kama ulimgusa, Yeye angetenda vivyo hivyo. Kwa hiyo nyosha mkono umguse usiku wa leo kwa imani yako.

154 Haikuwa. . .yeye. . .Vema, unasema, “Siko karibu vya kutosha kuweka mikono yangu juu ya vazi Lake.” Ni. . .Hilo halikuninii, hilo silo lililofanya jambo hilo, Yeye asingeweza kuhisi hilo, vazi la Kipalestina lina vazi la ndani, na joho kubwa linalopwaya. Mavumbi huingia chini ya joho hilo, hiyo ndiyo sababu walikuwa na kutawadha miguu, na kadhalika, kuondoa mavumbi miguuni mwao. Kwa hiyo, wao, va—vazi la Kipalestina likipwaya namna hiyo, kamwe hakugusa ninii. . . kugusa upindo huo.

155 Kwa nini Yeye hakuwahisi hawa wote waliokuwa wamemkumbatia? “Halo, Rabi. Nina furaha kukutana nawe, Kasisi,” na kadhalika. Kwa nini Yeye hakuwahisi? Walimgusa zaidi ya huyo mwanamke alivyofanya, bali Yeye aligusa. . . mwanamke aligusa upande wa ndani.

Kasema, “Nilihisi nguvu zikinitoka.”

¹⁵⁶ Siku chache baadaye akapitia kwenye birika la Bethesda, na kulikuwa na mtu aliyekuwa amelala pale aliyekuwa hawezi. Kulikuwako na watu wa kila namna pale, viwete, vipofu, vilema, waliopooza, kila namna ya—ya mateso, Yesu alitembea moja kwa moja kati yao wote, akiangalia kote, mpaka akamwona mtu amelala kwenye godoro; nadhani mngeliita hivyo. Sisi sote watu wa kusini tunajua godoro ni nini, sivyo? Nililelewa kwenye moja. Kwa hiyo, amelala kwenye godoro, amelala pale, naye hakuwa kiwete, kipofu, alikuwa na, hebu tuseme alikuwa na ugonjwa wa tezi dume, ama huenda alikuwa na TB, ulikuwa umedumaa, haungemwua, alikuwa ashakuwa nao miaka thelathini na minane.

Yesu akaangalia kote mpaka akampata, ndipo akasema, “Wataka kuwa mzima?”

¹⁵⁷ Akasema, “Bwana, sina mtu wa kunitia majini. Ninapokuja, mtu fulani huenda mbele yangu,” kwa maneno mengine, “hunitangulia kuingia majini,” mnaona, “mbele yangu, hushuka mbele yangu.”

Akasema, “Jitwike godoro lako, uende nyumbani kwako.” Mnaona? Ati nini? Biblia ilisema, “Kwa kuwa Yesu alijua.” Mnaona?

¹⁵⁸ Sasa, Yeye aliulizwa juu ya jambo hilo, Yohana 5, na, Yohana 5:19, alipoulizwa, Yeye alisema, “Amin, amin, nawaambia, Mwana,” ule mwili, “Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile *amwonalo* Baba analitenda. Kwa maana Baba anatenda kazi, nami ninatenda kazi hata sasa. Sifanyi chochote mpaka nione.” Basi kama aliliona, alimwona Baba, kwa ono, akitenda kazi. Mungu alimwonyesha kwa ono jambo la kufanya, Naye akaenda na kulifanya.

¹⁵⁹ Angalieni kule kufufuliwa kwa Lazaro, wakati alipokuja kwenye kaburi. Unaona pale kaburini, Yeye alisema, “Na—nakushukuru Wewe, Baba, tayari umenisikia Mimi,” alijua yaliyokuwa yanaenda kutukia, “lakini nasema kwa ajili ya hawa wanaosimama karibu: Lazaro, njoo huku.”

¹⁶⁰ Lazaro akafufuka. Loo, jamani! Hakika, kwa sababu alikuwa ameliona likitendeka. Alisema hakufanya lolote mpaka Baba alipomwonyesha. Kamwe hakusema lolote kuhusu nguvu kumtoka wakati huo. Huo ulikuwa ni muujiza mkuu jinsi gani kuliko yule mwanamke? Lakini mnaona huyo alikuwa ni Mungu akitumia karama Yake, huyo alikuwa ni mwanamke akitumia Mu-... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁶¹ ...lakini ilimbidi kuja wakati alipoweza. Kwa hiyo anakuja na mtungi wake wa maji, naye amehuzunika, labda akiwazia kile alichokuwa... kuhusu usiku uliotangulia, naye akashusha mtungi apate kuchota maji. Wakati alipoizungusha winchi namna *hii*, na kuuweka chini, aliangalia, akauweka, akamsikia

mtu fulani akisema, “Mwanamke, nipe maji ninywe.” Ndipo akageuka, na hapo aliketi Myahudi ameketi pale.

Sasa, yeye alikuwa ni Msamaria, akasema, “Si kawaida kwenu Wayahudi, Wewe ukiwa Myahudi hapa, kuniuliza mimi, mwanamke Msamaria.”

¹⁶² Alikuwa ni Jamaa mdogo. Vema, Yeye kweli alikuwa na umri wa miaka thelathini tu, bali Biblia inadai ya kwamba alionekana ana umri wa miaka hamsini. Mnajua hilo? Nadhani kazi Yake—Yake ilimtia mvi kidogo. Akasema, “Wewe,” katika Yohana Mtakatifu 6, akasema, “wewe ni mtu asiyezidi umri wa miaka hamsini, nawe unasema umemwona Ibrahimu?”

Akasema, “Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Mnaona?

Sasa, lakini alionekana ana hamsini, nadhani, kasema, “Wewe ni mtu asiyezidi umri wa miaka hamsini.”

¹⁶³ Sasa, lakini alipomwona Myahudi huyu ameketi pale, alisema, “Si kawaida Kwako, Myahudi, kuniuliza mimi, mwanamke Msamaria, kitu kama hicho, hatuna uhusiano sisi kwa sisi.”

Akasema, “Lakini kama ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe.”

Akasema, “Kisima ni kirefu.”

¹⁶⁴ Sasa, Yeye alikuwa akifanya nini? Itawabidi kuchukua neno langu kwa hili, Yeye alikuwa akiwasiliana na roho yake, mnaona, akijaribu kuitafuta roho yake. Mnaona, Baba alikuwa amemtuma huko juu, “Alikuwa na haja kupitia Samaria.” Lakini alipofika kule juu, hakujua la kufanya zaidi ya kungojea. Halafu huyu hapa. . .

¹⁶⁵ Aisee, jambo lile lile hapa usiku wa leo, Baba alinituma Beaumont, inanibidi kungojea nione yale atakayosema, si—si—sijui. Mnaona? Kungoja tu. Sasa, tuone baada ya kitambo kidogo kama Yeye alifanya hivyo au la. Mnaona?

¹⁶⁶ Ndipo basi, akaketi chini pale, na kuzungumza naye. Alikuwa akifanya nini? Akiwasiliana na roho yake, Naye akapata mahali shida yake ilipokuwa. Kuna mtu anayejua ilikuwa ni nini? Hakika. Alikuwa na waume watano, sita, hasa, alikuwa na waume watano, “Yule unayeishi naye sasa siye mume wako.” Vema.

Naye akasema, “Mwanamke, nenda kamwite mumeo, mje hapa,” baada ya Yeye kuona shida yake.

Akasema, “Sina mume yeyote.”

¹⁶⁷ “Loo,” kasema, “umesema kweli.” Kasema, “Ulisema kweli, kwa sababu umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa si wako. Kwa hiyo, basi ulisema kweli.”

168 Alifanya nini? Hakuwa kama baadhi ya hao makasisi wenye kujiita wenyewe huku ukosi wao umepinduliwa, pamoja na theolojia yote nchini. Alijua mengi zaidi kumhusu Mungu kuliko nusu ya wahubiri Marekani wajuavyo, naye akiwa katika hali *hiyo*. Akageuka, akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii.” Amina. Kasema, “Tunajua, sisi Wasamaria, tunajua ya kwamba hiyo itakuwa ndiyo ishara ya Masihi.” Hiyo ni kweli? “Tunamjua Masihi, aitwaye Kristo, atakapokuja, Yeye atatwambia mambo haya, lakini u Nani Wewe?” Loo, jamani!

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

169 Ndugu, alikunywa kutoka kwenye Chemchemi mpya wakati huo. Akaacha mtungi huo wa maji pale, akakimbilia mjini mbio alivyoweza. Sikilizeni kile alichosema, “Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?”

170 Nayo Biblia ilisema watu wa mji huo walimwamini Kristo kwa sababu ya neno la huyo mwanamke. Kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi jana, ilikuwa ni ishara ya Masihi leo. Hiyo ni kweli?

171 Sasa, nukuu moja zaidi, sasa, ni ndefu kidogo, lakini samahani kwa dakika moja tu zaidi. Hili ni kanisa, nadhani si lazima walifunge kwa wakati fulani. Ninawatakeni mpate nukuu hili moja zaidi, kisha tutafunga.

172 Sasa, mliona, ishara hiyo kamwe haikufanywa mbele ya Mmataifa? Hawakuwa wakimtazamia. Ilikuwa imeondoka... Ilikuwa ni ishara kwa Myahudi na kwa Msamaria, lakini Injili hata haikuwafikia Mataifa mpaka Petro alipopanda na kuwahubiria, Matendo 10:49. Mnaona? Walikuwa makafiri. Kwa hiyo, Yeye hakuwajia wasioamini, alikuja na kuwaonyesha ishara Yake ya Masihi waaminio.

173 Sasa sikilizeni kwa makini, nanyi wasikilizaji wa nje, jivikeni mawazo ya kiroho sasa, kwa sababu itawabidi kusoma katikati ya mstari hapa, kisha nitafunga.

174 Sasa, wakati alipokuwa hapa duniani, walimwuliza ishara ya kuja kwa mwisho wa ulimwengu. Naye akasema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma,” kwanza Yeye alisema, “za Nuhu,” ile mvua. Basi aliposema juu ya Nuhu, Yeye aliendelea na kutoa yaliyotukia katika siku za Nuhu, kuhusu maadili ya watu, jinsi wangukuwa watovu wa uadilifu, kuhusu walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa. Ndipo anakuja Sodoma, akasema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

175 Sasa sikilizeni kwa makini, sasa angalieni, Ibrahimu aliwawakilisha wateule na watu walioitwa watoke. Daima kuna matabaka matatu ya watu, yakumbukeni. Lutu aliwakilisha kanisa vuguvugu, la kawaida; Wasodoma walikuwa ni walimwengu; naye Ibrahimu alikuwa amejitenga na

kutokuamini huko kwote, naye alikuwa ametoka. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... Kanisa teule. Sasa kumbukeni, katika wale Malaika watatu waliokuja kukutana na Ibrahimu, walikuwa ni watu watatu, nao walikuwa ni Malaika watatu wa Mungu, Mmoja wao alikuwa ni Mungu, Mwenyewe.

¹⁷⁶ Mhudumu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, “Humaanishi kusema huyo alikuwa ni Mungu?”

¹⁷⁷ Nikasema, “Biblia ilisema ilikuwa ni Mungu. Ibrahimu alimwita Bwana, herufi kubwa B-w-a-n-a, Elohimu. Anapaswa kujua, yeye ndiye aliyekuwa akizungumza Naye.”

Akasema, “Vema, huo ulikuwa ni thiofania tu.”

Nikasema, “Thiofania hauli ndama wala kunywa maziwa ya mtindi.” Hiyo ni kweli. Alikuwa ni Mungu! Biblia ilisema alikuwa. Yeye alikuwa ni Mungu, ndugu.

Hawa Malaika watatu, yeye alisema, “Mbona, unamaanisha walikuwa ni Malaika?”

Nikasema, “Hakika.”

“Wamevaa nguo zilizojaa mavumbi, na wakila?”

Nikasema, “Hakika. Hujui tu jinsi Mungu wetu alivyo mkuu.”

¹⁷⁸ Alitaka kushuka kuja kuchunguza hali ya mambo huko Sodoma. Kwa hiyo, ninaweza kuwazia: Mwili wetu umeumbwa kwa kitu gani? Elementi kumi na sita, potashi, na kalisi, petroli, nurulimwengu. Alinyosha tu mkono na kuchukua elementi kumi na sita, akafanya, “*Whiu!*” akazipulizia pamoja, na kusema, “Njoo hapa, Gabrieli. Ingia *hapa* ndani.” Hakika. Akapuliza moja kule kwa ajili ya Mikaeli, akaupulizia mwingine kwa ajili Yake Mwenyewe, akaingia tu, akashuka.

¹⁷⁹ Loo, nina furaha sana ninamjua! Mojawapo ya siku hizi wakati mwili wangu ni mavumbi tu yanayopeperushwa duniani, Yeye atafanya, “*Whiu!* Rudi.”

¹⁸⁰ Nina furaha sana kumjua Mungu wa namna hiyo, kulipulizia tu pamoja, hivyo tu, “Njoo, sasa, nilikuahidi. Ulikuwa mwaminifu kwa mambo machache, nitakufanya mtawala juu ya mengi.” Mnaona? Mrithi wa vitu vyote kwa njia ya Kristo. Yeye hatambui tu kwamba Yeye ni Nani, jinsi alivyo mkuu.

¹⁸¹ Naye akashuka. Nami nawatakeni mwone, wawili wa hao Malaika, Billy Graham wa kisasa, na kadhalika, walitoka wakaenda kuwahubiria Wasodoma. Hiyo ni kweli? Na kulikuwa na mwujiza mmoja tu waliofanya, kuwapofusha, na kuhubiriwa kwa Injili huwapofusha wale wasioamini. Lakini aliwaonyesha ishara hiyo huko chini, Injili ikihubiriwa, “kutoka.”

¹⁸² Hakumwita Ibrahimu atoke, tayari alikuwa ametoka. Loo, nina furaha sana! Ibrahimu aliwakilisha Kanisa teule, Kanisa

lililoitwa litoke. Lakini Mmoja alibaki nyuma na Ibrahimu, Naye akafanya ishara. Ninawatakeni mwone ni ishara ya namna gani aliyolifanyia Kanisa teule.

¹⁸³ Sasa, mnaona, walikuwa wamehubiriwa Injili watoke mahali hapo, huko chini, bali Huyu alibaki nyuma pamoja na Ibrahimu. Kasema, sasa kumbukeni, Yeye alikuwa ni Mgeni, alikuwa na mavumbi nguoni Mwake, alitoka Nchi ya kigeni, naam, *mbali* sana, Naye akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” Alijuaje kwamba alikuwa ameo? Na alijuaje alikuwa na mke jina lake Sara? “Ibrahimu, yu wapi Sara mkeo?”

¹⁸⁴ Sasa, Biblia inasema kabisa ya kwamba yeye alisema, “Yuko hemani nyuma Yako,” nyuma ya Malaika. Huyu Malaika alikuwa ni Mungu katika mwili wa mwanadamu. Angalieni, kasema, “Yuko hemani nyuma Yako.”

Angalieni hili: “Katika muhula wake nitakuzuru.”

¹⁸⁵ Ndipo Sara akacheka moyoni mwake, sio kwa sauti kubwa, akafanya, “*Hmmph!*” ndani ya hema. Na huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema, Yeye akasema, “Kwa nini Sara akacheka?”

¹⁸⁶ Ni telepathia ya namna gani hiyo? Ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni ishara kwamba ulikuwa tu tayari kuteketezwa. Sasa, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma,” na ulimwengu uko katika hali ya Sodoma sasa. Kabla tu ya Moto kushuka, Malaika wa Bwana anarudi na kuishi katika mwili wa mwanadamu, na anafanya ishara iyo hiyo kuwapa Mataifa, ishara ile ile ya Masihi aliyowapa Wayahudi na Wasamaria. Mnaliona? Hana budi kufanya hivyo.

¹⁸⁷ Kama akiliacha Kanisa hili liendeleo na theolojia pekee, Yeye angewapa kibali na ishara ambayo hakuturuhusia. Na endapo Mungu ni yeye yule, Naye ni yeye yule, atafanya vivyo hivyo na kutenda vivyo hivyo kwa kila mmoja wa watoto Wake; na kwa kila kizazi hana budi kuwa vivyo hivyo. Kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara Yake katika siku hiyo kwa Wayahudi, Wasamaria mwishoni mwa siku yao, huku ni kumalizia kwa siku yetu...

¹⁸⁸ Injili inarudi tena kwa Myahudi hivi karibuni sana, anaingojea sasa hivi, anangojea tu ile ishara ionekane kwake, ndipo basi Yeye atarudi, ambapo Eliya na Musa watafanya hivyo katika Ufunuo 11, kama mjuavyo.

¹⁸⁹ Sasa, lakini basi Kanisa la Mataifa liko kwenye wakati wa mwisho. Hiyo ni kweli? Tunaamini jambo hilo, ya kwamba huu ni wakati wa mwisho, na kuteketezwa kwa Sodoma kumekaribia. Vema, bomu la atomiki tayari liko kwenye kibanda huko ng'ambo huku jina la ulimwengu limeandikwa juu yake. Hiyo ni kweli. Utateketezwa, usijali kuhusu hilo. Utateketezwa, uko tayari sasa hivi kurushwa wakati wowote. Acha tu mwehu fulani avute ninii... Moja ya makombora haya, moja ya siku

hizi, litaingia kwenye skrini ya mtu fulani, ndipo basi kila mtu ataanza kuyaachilia katika kila taifa, basi imewasili. Lakini kabla hilo halijatukia, Kanisa linaenda Nyumbani, Kanisa linaenda Nyumbani, kamwe halitakuwa katika hayo. Sasa, mnaelewa?

¹⁹⁰ Lakini kwenye wakati huo tu wa mwisho ishara hii itatokea tena. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... alikuwa Sodoma. Kanisa teule, si lile vuguvugu, wana yao, bali Kanisa teule, lililoitwa litoke (Mnaweza kusoma katikati ya mistari? Mnaona?), Kanisa lililoitwa litoke litapokea ishara hiyo, na hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi. Ni ishara ya Masihi miongoni mwetu.

¹⁹¹ Sisi si Masihi, bali Masihi anaishi ndani yetu, ambalo *Masihi* maana yake ni, “Aliyetiwa Mafuta,” na hana budi kututia mafuta sisi sote. Kama akimtia mafuta mmoja kwa ishara, na huyo mwingine haiamini, ingefaa nini? Haina budi kuwa ni sisi sote pamoja. Na, pamoja, kama Yesu Kristo atatokea hapa usiku wa leo, na kufanya ishara zile zile za Masihi alizofanya huko nyuma mbele ya Myahudi na Msamaria, ungempokea kama Mwokozi wako na kama Mponyaji wako? Je, ungempokea? Hilo ni tamshi kubwa. Mpokee kama Mwokozi wako. Sasa, kumbukeni Yeye hawezi kuponya. Jambo lake la kwanza, Yeye anakutaka uliamini.

¹⁹² Ana watu waliotawazwa hapa kufanya hivyo, lakini mbali na hayo, Mungu aliweka ofisi nne zilizoitwa na Mungu Kanisani, Mitume, ambao kwa kweli ni *mmishenari*. *Mmishenari* maana yake ni, “mtu aliyetumwa,” *mtume* maana yake, “mtu aliyetumwa.” Vema. *Mmishenari* ni *mtume*. Vema. Mitume, manabii, walimu, wainjilisti, na wachungaji, ninamaanisha watano badala ya hao wanne. Ni ofisi tano ambazo Mungu aliagiza na kuziweka Kanisani. Mnaamini hilo? Vema. Basi kama tunaamini kuna mitume, manabii, walimu, wachungaji, wainjilisti, kuna ofisi nne.

¹⁹³ Katika kila kanisa la mahali hapo kuna karama kumi na mbili, ama, karama tisa za kiroho, Wakorintho wa Kwanza 12, karama tisa za kiroho zinazotenda kazi kupitia ule Mwili. Mnaona, Mungu aliweka kila maandalizi ya kulidumisha Kanisa hilo safi liwezavyo kuwa, bila waa wala kunyanzi. Uh-huh. Tuko kwenye wakati wa mwisho, watu wa Mataifa, tuko kwenye wakati wa mwisho.

¹⁹⁴ Sasa, ninaamini ya kwamba Yesu Kristo angali ndiye Masihi. Ninaamini kama alikuwa ameshuka kule kabla ya Sodoma, na kusimama kwenye Kanisa teule... Kumbukeni, Yeye kamwe hakushuka kwenda Sodoma, alikuja kwa Wateule, kwa Kanisa. Karama hizi hazipelekewi...

Mnasema, “Kwa nini usiingie kwenye vituo vikubwa-vikubwa?”

¹⁹⁵ Vituo vikubwa-vikubwa ni watu wa Mungu. Uh-huh. Huja makanisani, mahali padogo. Si lazima liwe lililopambwa, na... Hivyo ndivyo ilivyo. Yesu hakuwa mtu wa maonyesho.

Walimwambia, “Kwa nini usije kwa Kayafa? Kwa nini usiende huku Yerusalemu, ukajionyeshe?”

Akasema, “Wakati wenu ni sikuzote, wangu haujaja.” Yesu hakuwa mtu wa maonyesho. Hakuajionyesha.

Kasema, “Unaishi katika kundi hilo la watakatifu wanaojibingirisha kule chini, kundi la wavuvi, na kadhalika, panda huku kwa watu wa tabaka la juu.”

¹⁹⁶ Alikuwa kwa wale ambao Mungu alimtuma kwao. Nao... Tunafanya mambo haya kwa sababu tunaongozwa kufanya mambo haya, Mungu huwaongoza watoto Wake. Natumaini mlilipata hilo.

¹⁹⁷ Sasa, kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, basi kuhusu uponyaji, mtu yeyote anayekuja na kusema wanaweza kukuponya, hilo ni kosa, hilo si la kimaandiko, Yeye tayari amekuponya. Kama mtu akisema anaweza kukusamehe dhambi zako, amekosea, tayari zimesamehewa. Unaona? Tayari zimesamehewa, inakubidi tu kukubali jambo hilo.

¹⁹⁸ Lakini kuna wachungaji wanaoweza kukuongoza, kuna walimu wanaoweza kufundisha, kuna wainjilisti, kuna mambo mengine, na kuna manabii, na mambo haya yote mbalimbali, na katika siku ya mwisho ishara ya Masihi ilikuwa ionekane Kanisani.

¹⁹⁹ Sasa kumbukeni, ni wangapi waliopata kuona ile picha iliyopigwa hapa Houston? Naam, bwana, ni wote... Iko hapa mahali fulani sasa, nadhani. Mnaona? Sasa, imepigwa kote nchini, jambo lile lile kila wakati. Mnaona? Sasa, ni Nguzo ya Moto.

²⁰⁰ Sasa, wakati Yesu alipokuwa duniani, ni wangapi wanaoamini ya kwamba Yeye alikuwa ni yule Malaika aliyekuja pamoja nao nyikani? Alisema alikuwa. Uh-huh. Yeye ni Malaika wa agano. Naye... hapa Yeye alisema, “Nilitoka kwa Mungu, nami naenda kwa Mungu.” Hiyo ni kweli? Ndipo alipokufa, akafufuka, na kutoka kaburini, basi siku moja Paulo, ama, Sauli alikuwa akienda zake Dameski, ndipo Nuru ikambwaga chini, Nuru nyingine. Petro, iliingia jengoni, gerezeni, na kumtoa nje. Basi Nuru hii ikaja kwa—kwa, ikambwaga chini Sauli magotini mwake, Naye akasema, “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi.”

Akasema, “U nani Wewe, Bwana?”

Akasema, “Mimi ni Yesu. Nilitoka kwenye Nguzo ya Moto, ninarudi kwenye kitu kile kile nilichokuwa.” Hiyo ni kweli? Sasa, Biblia ilisema hiyo ni kweli.

²⁰¹ Vema, basi, kama hii ndiyo aina sahihi... Kama ni Nguzo ile ile ya Moto, basi itafanya mambo yale yale aliyofanya. Kama

Nguzo hiyo ya Moto iliyo pamoja nasi usiku wa leo, kama huyo ni Roho wa Yesu Kristo, itatenda ndani yako jinsi ilivyotenda ndani Yake. Mnaona ninalomaanisha? Basi hilo linalifanya kweli. Sasa, kama tunaweza kumwona akijitokeza jukwaani na kutenda kama alivyotenda hasa, kila mmoja wenu angeamini ilikuwa ni Bwana Yesu?

Na tuombe.

²⁰² Baba wa Mbinguni, inaonekana kana kwamba ningeweza kuzungumza usiku kucha, kundi zuri sana la watu, mioyo yao kama tu, kama tu vipokezi, Bwana, wakivuta tu kutoka kwako. Jinsi ninavyopenda hilo, Baba! Na kujua ya kwamba ninaamini ya kwamba hili ni la Ibrahimu, lile Kanisa, Lililoitwa litoke, Kanisa teule likiwa na kweli ya Injili, likiihubiri!

²⁰³ Wengi, Bwana, huenda wasiweze kupenya katika ishara mbalimbali, kama nilivyosema, bali hawawazuii wengine kufanya hivyo. Bwana Mungu, wanakuamini Wewe, wanaamini Ne—Neno. Wengi wao walikuwa wakiihubiri nilipokuwa mvulana mdogo, na hapa, nikisimama hapa usiku wa leo mbele ya watu kama hao, watu wanaoshikilia kweli ya Injili kifuraha mwao! Wanawake, wako na wake zao hapa, wapendwa wao, watoto, wagonjwa wao na wahitaji. Waliitetea hii, wao, miaka mingi iliyopita walikuwa wametengwa, wamefukuzwa kutoka kwenye makanisa mengine, walisimama pembeni wakiwa na tari mkononi mwao, baadhi ya wanawake hata hawana pesa za kutosha kununua soksi ndefu, walisimama pale wameshika gita kuukuu mikononi mwao, na kuipiga, na kuutangaza Ujumbe.

²⁰⁴ Mungu, saa imewadia sasa, saa imewadia. Waliitengeneza njia, wakanyosha mapito nyikani. Tunaomba ya kwamba Masihi wa Mungu atapitia njia hiyo usiku wa leo, ashuke katikati yao. Tuonyeshe, Bwana, Uwepo Wako, “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu,” Yesu huyu waliyenena habari zake, na akastahimili mateso ya Jina Lake.

²⁰⁵ Bwana, onekana katikati yao usiku wa leo, na uonyeshe ya kwamba Wewe ungali ni Masihi yeye yule, ya kwamba Wewe huja, ulifufuka katika wafu, na unaishi katika Kanisa Lako. Wewe Ndiwe uliye pamoja nao wakati wote. Tujalie, Baba. Jalia tu tukuone Wewe, na kila mmoja wao ataamini, Baba. Tunajikabidhi Kwako. Tunaomba ya kwamba utatujalia baraka hii, kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁰⁶ Sasa, nitawaomba sasa, kama kila mtu atabaki tu kitini mwao sasa, kwa dakika chache. Sasa, ningeweza kusimama hapa na kuzungumza juu ya mambo haya, lakini sasa, je, ni ya kweli? Hilo ndilo jambo linalofuata. Je, ni ya kweli? Wengi wenu hamjawahi kuiona, bali mngali mnaiamini. Mnaona? Mngali mnaiamini, kwa vyovyote vile. Lakini sasa, sijui ya kwamba atafanya hivyo, bali ninatumaini ya kwamba atafanya hivyo. Na

kama akifanya na kutenda vile vile alivyofanya alipokuwa hapa duniani. . .

207 Sasa, njia pekee anayoweza kufanya ni mimi kujisalimisha Kwake, nijisalimishe tu, na kujiondoa njiani, nawe ujiondoe njiani. Sasa, hiyo ndiyo njia pekee. Pamoja basi tutamwona Masihi. Mimi kujisalimisha tu hakutoshi, ninii tu, inakubidi kujitolea, nami sina budi kujitolea, na pamoja Masihi anatenda kazi miongoni mwetu, kwa sababu sisi ni watu Wake, waliochaguliwa, waliotakaswa kwa Damu Yake.

208 Roho Mtakatifu anakaa ndani yetu, Naye ni ninii tu, kama vile kile kifungo kidogo kikiwa ni Roho Mtakatifu, anapokuja katika mfano wa ubatizo, ndipo anaanza tu kuenea. Tunapoondoa mizizi yote ya uchungu na uovu kutoka kwetu, Mungu huchukua tu mamlaka na kuanza kutenda kazi.

209 Angalia maikrofoni hii, maikrofoni hiyo ni—ni bubu bila kitu cha kuzungumzia ndani yake. Hiyo si maikrofoni inayozungumza, huyo ni mimi. Kwa hiyo isingeweza kuwa ni mimi ninayezungumza, ingekuwa ni Yeye, maana... Mnaona? Haiwezekani kuwa ni wewe unayenena, ni Yeye. Unaona? Hatujui lolote la wakati ujao. Hatujui... Sijui... .

210 Hakuna mtu, tangu nimeketi hapa nikiangalia katika jengo hili, ambaye ninamjua, isipokuwa iwe ni Ndugu Moore na Ndugu Brown, hapa, Ndugu Mercier, aliyeketi nyuma yangu, mwanangu, aliyeketi pale.

211 Huenda nikawajua baadhi yenu wanaume kama ningeninii... ungeniambia jina lako lilikuwa nani, ama kuniambia mahali tulipokutana, sijui, kuna uwezekano mkubwa wa kuwajua wahubiri. Ni wangapi huko nje katika kusanyiko hili wanaojua ya kwamba hatufahamiani? Inua mkono wako. Sijui lolote kukuhusu, sijui lolote kuhusu kudhurika kwako, magonjwa yako, au matatizo, ama kadhalika? Mnaona? Kila mahali.

212 Vema, ngojeni kidogo, ninaamini m—mlisambaza kadi. Vema. Tutajaribu kadi za maombi kwanza. Sasa, hatuwezi kuleta wengi sana hapa juu kwa wakati mmoja. Ilikuwa ni ipi, Billy? Ilikuwa ni A? Kadi ya maombi A. Sasa, hiyo ni A, moja hadi mia moja. Itatubidi kuanzia mahali fulani hapo. Tunaanzia mahali fulani, labda usiku wa leo, kesho usiku, mahali pengine, usiku ujao, mahali pengine. Kwa sababu tu tulikuwa tukifanya hivyo, tungeanza... .

213 Ni—nilitoa kadi zangu, wengi wenu mnakumbuka, hapa chini, nilikuwa... Nilimpa mwenzangu wakati mmoja, wakamkamata akiuza kadi za maombi wapate kumwingiza mtu kwenye mstari wa maombi, nilisimamisha hilo upesi sana, nikamweka ndugu yangu azisimamie. Sasa, ndipo mwanangu akaja, nikamweka apate kuzigawa, na watu waaminifu.

214 Kisha ningekuwa, kwa kitambo kidogo ningewafanya watoto wadogo kama *hawa* wasimame, kama vile ningekuwa na Junior hapa, ningesema, “Wewe simama, na uanze kuhesabu, Junior, na popote utakapoachia kuhesabu, hapo ndipo nitaanza kuitia.” Huh! Amini usiamini, sisi tungali wanadamu. Mama alimfanya Junior kusimama moja kwa moja kwenye namba yake, mnaona, papo hapo ilipokuwa. Kwa hiyo nisingeweza kufanya hivyo, malalamishi yanaibuka. Kwa hiyo, usiku mmoja katika maombi Roho Mtakatifu alisema tu. . .

215 Halafu basi, jambo la kwanza ninalofanya. . . Mkutano wa kwanza, nilishuka, nikawapa wote, kila mtu kadi ya maombi, nikampa kila mchungaji kadi mia moja za maombi kuwagawia nanii wake. . . Ninaamini hivyo ndivyo tulivyofanya hapa mara ya mwisho, ninaamini, katika mkutano wa Beaumont. Lakini mtu wa kwanza alipoliingiza kundi lake, hilo lilitosha kwa hao wengine. Mnaona? Kwa hiyo usingeweza kufanya hivyo.

216 Basi njia pekee, ya haki, tuliyoona ya kufanya hivyo ilikuwa ni kuzigawa kila siku. Kila. . . Na kwamba, kama jamaa fulani, kama umeombewa, ilikubidi kuhudhuria mkutano wa kwanza, la sivyo uko nje. Jamaa akija siku ya pili, asingeweza kupata kadi ya maombi, siku ya tatu, haidhuru ilikuwa nini, niliwajibika kuwaombea kwanza. Mnaona? Kwa hiyo hawakuingia kwenye mstari wa maombi.

217 Kwa hiyo sasa kile tunachofanya ni kuzigawa, tumefanya hivyo kwa miaka mingi, tunazigawa, zote pamoja, kila siku. Ndipo usiku huo tunashuka, popote tu Roho Mtakatifu anapoanza kuhusika nami. Wakati mwingine nilihesabu ni wangapi walio kwenye *huu*, ni wangapi walio upande *huu*, na kuwagawanya kwa upande *huu*, kuanza namna hiyo, mahali popote, hatujui, popote tu Roho Mtakatifu anapoliweka niani mwangu, basi ninajua.

218 Huyu mtu anayekuja kuwapa kadi ya maombi, hao wavulana watakuja mbele zenu, kwanza, na kuchukua kadi hizi za maombi na kuzichanganya, kila moja, mbele zenu, kisha watoke na kuzigawa. Huenda ukapata namba saba, wewe upate arobaini na tano nawe upate mia moja, na namna hiyo, mtu aliye karibu nawe. Zote zimechanganyishwa, kwa hiyo basi ninaposhuka, basi hilo limekaguliwa maradufu, hata hakuna mtu anayeweza kusema, “Vema, wanauza kadi za maombi kumwingiza mtu fulani kwenye mstari wa maombi.” Hatuwezi kufanya hivyo, mnaona, zote zimechanganyishwa tu pamoja.

219 Ndipo Roho Mtakatifu anatoka moja kwa moja, na kuwachukua hao huko nje ambao hata hawana kadi ya maombi, mnaona, anatabiri mambo. La, mnaona, ni wazo tu la kumleta mtu hapa juu, kusudi nipate upako, nawe upate upako, umpokee Roho Mtakatifu.

220 Kwa hiyo usiku wa leo hebu tuanze tu kutoka namba moja kwanza, kwa kuanza, tuone ni wangapi tunaoweza kuwasimamisha. Namba moja, ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja? Iwapo huwezi kutembea sasa, kadi yako itakapoitwa, baadhi ya ndugu hapa watakusaidia. Kadi ya maombi A, namba moja. Iko wapi? Angalia kadi yako ya maombi sasa. Kadi ya maombi A, namba moja. Mna hakika mligawa kadi za maombi? Loo, mimi. . . Vema. Hebu mama huyo aje hapa kama anaweza kutembea, kama anaweza, anaweza kusimama.

221 Namba mbili. Ni nani aliye na namba mbili? Inueni mikono yenu upesi tupate kuona. Papa hapa. Njoo papa hapa, Dada. Sasa, kama huwezi kusimama, inua tu mikono yako, nasi tutakuja tukubebe. Unaona? Namba mbili, namba tatu. Waweza kuinua mkono wako? Huyu mama? Namba nne, namba nne. Tunafanya hivi kudumisha utaratibu.

222 Hebu niwaonyeshe jambo fulani: Ni wangapi hapa ndani wanaotaka kuombewa, inueni mikono yenu, kote jengoni. Vema. Nani anataka kuwa wa kwanza? Haya basi. Mnaona? Huna budi kufanya hivyo. Inakubidi tu, kudumisha utaratibu.

223 Namba moja, mbili, tatu, nne. Ni nani aliye na kadi ya maombi nne? Vema, njoo hapa, mama. Namba tano, ni nani aliye na kadi ya maombi namba tano? Njoo papa hapa, mama. Nyote pageni mstari sasa. Namba sita. Namba sita, hapa nyuma. Vema. Namba saba. Kadi ya maombi namba saba. Waweza kuinua mkono wako? Kadi ya maombi saba.

224 Angalia, mtu fulani awaangalie watu hawa, kuna mvulana mdogo kiwete aliyeketi hapa, na wanawake wawili, na watatu hapa kwenye viti vya magurudumu, angalieni kadi zao za maombi sasa. Mnaona?

225 Namba saba. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba. Namba nane, namba nane, waweza kuinua mkono wako kama anaweza? Huko nyuma kabisa. Namba tisa. Vema. Kumi, namba kumi, kumi na moja. Hiyo ni kweli, hiyo ndiyo njia. Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne. Vema. Kumi na nne. Iko huko? Kumi na tano, kumi na tano, kumi na sita. Vema. Kumi na saba, kumi na nane. Niliikosa. Kumi na nane, kumi na nane. Kadi ya maombi kumi na nane.

226 Vema, hizo zinatoshia. Hebu wasimame papo hapo kwa dakika moja. Tunaweza kuanza kuwaombea hawa basi. Sasa, kumbukeni, hapo kadi yako ya maombi ikiitwa, ingia moja kwa moja mstarini. Vema.

227 Sasa, sasa, hapa, Dada, la, wewe—wewe ingia, loo, ni, loo, una namba gani hapo? Kumi na nane. Rudi moja kwa moja hapo mstarini papo hapo, moja kwa moja huko nyuma, hao wavulana watakuweka mstarini. Hapa, moja kwa moja kupitia hapa, pitia hapa, mama, karibu huku, njoo huku.

228 Sasa, ni wangapi hapa ndani wasio na kadi ya maombi, na hata hivyo wewe ni mgonjwa, unataka Mungu akuponye? Vema, inua mkono wako. Vema. Ninajaribu kupata fu—fununu uko wapi. Um-hum. Karibu kwa jumla, kila mahali. Vema. Sasa, kama huna kadi ya maombi, nitakwambia kile ninachotaka ufanye, wewe usiye na kadi ya maombi, fanya hivi: Kama Bwana akianza kuwaponya watu jukwaani, basi angalia huko juu, na useme, “Bwana, aliniambia . . .”

229 Na hebu tuwaulize hawa wahudumu hapa. Je, Biblia inasema sasa ya kwamba Yesu sasa, katika Kitabu cha Waebrania, ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Hiyo ni kweli? Vema, basi, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, kama ungemgusa, Yeye angetendaje? Vile vile alivyofanya jana, kama ni yeye yule jana, leo. Ndipo Yeye . . .

230 Sasa, hilo halitufanyi kuwa Yesu. Mnaona? Hilo linatufanya tu watumishi Wake. Mnaona? Sisi ni vyombo vyake alivyo navyo, akitenda kazi kupitia sisi. Yeye—Yeye huwatumia wanadamu kama vyombo Vya—Vyake vya kufanyia kazi. Hiyo si ni kweli?

231 Vema. Ninataka kila mtu ukae mahali pako, nyamaza kabisa, endelea kuomba. Sasa, sisemi kwamba itatendeka. Sasa kumbukeni, kama mimi . . . Hebu tuone, ni wapi? (Ndugu Jack, msaidie, msaidie anapokuja. Vema, hapa, yeye, hebu aje huku sasa, aje huku.)

232 Sasa, sasa watu hawa hapa, sasa, kila mmoja kwenye mstari wa maombi, ninataka kumwangukia kila mmoja wao, sasa, wote ni wageni kwangu, siwajui. Endapo hatufahamiani nanyi nyote, inueni mikono yenu, yaani siwajui, sijui lolote kuwahusu, wala chochote kile. Vema. Sasa, mleteni mama huyu hapa kwangu. Mnaweza kunisikia vizuri? Sasa, wakati mwingine wakati huo upako unapoingia, si—sijui ninazungumza kwa sauti kubwa jinsi gani. Mnaweza kunisikia vizuri, huko nyuma? Mfumo wa sauti. Kama nilikuwa nikizungumza hivi, mngeweza kunisikia bado? Mnaona?

233 Sasa, hili si ni jambo zuri sana? Hapa Biblia hii haina budi kuonekana kuwa ni kweli, ama si kweli; ahadi za Mungu hazina budi kuonekana kuwa ni za kweli, ama si kweli. Sasa, hawa hapa watu hawa walioinua mikono yao kwamba hawanijui, wala mimi siwajui; nyote mmeinua mikono yenu.

234 Sasa, nakwambia, kama una shaka hata kidogo, sema tu, “Bwana Yesu, mtu huyo hanijui, nami ninajua yeye ni mwanadamu tu. Lakini nitagusa vazi Lako, maana sina kadi ya maombi, nitagusa vazi Lako, kisha umgeuze na kunena nami, kama yule mwanamke aliyegusa vazi Lako, unene nami, na ndipo hilo lita—litanishawishi maishani mwangu mwote. Mnaona? Ninakuomba tu ufanye hivyo kama akitiwa mafuta.” Sasa, ungemwona Yesu? Ungemwonaje? Anapotembea kupitia kwetu. Sasa iweni katika maombi.

235 Sasa, sininii... Sasa, ninaposema iweni na kicho na utulivu, simaanishi... Wakati—wakati tunaposimama hapa, mnaona, ninaangalia, mtu yeyote asipige picha, maana ni Nuru.

236 Jumapili iliyopita, ilikuwa juma moja lililopita, Nguzo ii hii ya Moto ilisimama kanisani mwangu kwa dakika kumi na tano, mamia ya watu walisimama pale wakilia, wakipiga magoti, na kila kitu, ikasimama papo hapo, dakika kumi na tano, moja kwa moja mbele ya kusanyiko lote, wakaiangalia.

237 Ndugu Gene, ulikuwa pale, sivyo? Ndugu Leo? La, hebu tuone, ulikuwa huku chini, hiyo ni kweli, ulikuwa huku chini kusini. Ndugu Gene, baadhi ya... Ndugu Sothmann, anakusudiwa kuwa hapa mahali fulani, Ndugu Fred Sothmann. Mko wapi nyote, ndugu? Mahali fulani, hapa. Walikuwepo. Naam, huko nyuma. Tukisimama pale, tukaiangalia kwa dakika kumi na tano, ikisimama, papo hapo mbele yetu namna hiyo, tukiiangalia.

238 Ninatumaini ya kwamba itajionyesha Yenyewe tena hapa Beaumont kwa ajili yenu jamaa hapa. Kumbukeni, ni Nuru ile ile iliyowafuata wana wa Israeli, ni ile ile iliyombwaga chini Sauli, iliyoingia gerezani, ni Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.”

239 Sasa, Baba wa Mbinguni, huu ni umbali ambao wanadamu wanaweza kwenda. Sasa tuna—tunakiri dhambi zetu, kutokuamini kwetu kwote, nasi tunaomba ya kwamba Wewe utakuja pamoja nasi usiku wa leo, kwamba maneno haya na ahadi... Sasa, Wewe uliahidi, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Nami nimejaribu kuwaonyesha hilo usiku wa leo, Baba, ya kwamba sisi ni Mataifa, huu ulikuwa ni wakati ulipokuwa ukija kwa ajili ya Bibi-arusi wa Mataifa, mwisho wa wakati wa Mataifa.

240 Niliwaambia, na kuonyesha kutoka kwenye Biblia usiku wa leo, jinsi ulivyojithibitisha Mwenyewe kuwa Masihi wa watu kwa Wayahudi, Masihi kwa Msamaria. Sasa, Bwana, onyesha ishara ile ile ya Masihi, usiku wa leo, ya kwamba Wewe hujafa bali unaishi, na Wewe uko pamoja na watu Wako, kwa Mataifa, kwa kuwa tukiwa wafu katika Kristo sisi ni Uzao wa Ibrahimu, Bwana, nasi ni warithi pamoja naye katika ile ahadi.

241 Jalia Roho Mtakatifu aje, usiku wa leo, na kuchukua miili ye—yetu, kanisa hili lote, katika umilikaji, kuondolee mbali kutokuamini kwote miongoni mwetu, na jalia Maandiko yalizonukuliwa usiku wa leo, “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu,” ndipo wakapata shauku ya mioyo yao, jalia tupate jambo lile lile usiku wa leo, kwa sababu imeandikwa, “Ombeni, nanyi mtapata.” Tunalikabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁴² Sasa, hatuwajui watu hawa. Simjui mama huyu, anaonekana, nadhani, kuwa na umri mkubwa zaidi, labda, kuliko mimi. Na hakika sikuja hapa kumdanganya maskini mwanamke huyu, mwenye mvi. Nina mama nyumbani, anayeomba usiku wa leo, ambaye ninashukuru kwa ajili yake, hapana shaka huyu ni mama wa mtu fulani.

²⁴³ Sasa, tunakutana kabisa kama Yohana Mtakatifu 4. Huyu hapa mwanamke, wewe hunijui, sikuji. Sasa, tuliinua mikono yetu, si—sikuji, wala wewe hunijui. Sasa sisi hapa.

²⁴⁴ Sasa, wakati Yesu alipokutana na mwanamke ambaye hakuwa amemwona hapo kabla, kwenye kile kisima, mji wa Samaria, kisima cha umma, ni katika mandhari ndogo, kitu kama hiki, nao walikutana kwa mara ya kwanza, naye aliongea naye dakika chache mpaka akaona shida yake ilikuwa nini, kisha akamwambia shida yake ilikuwa ipi.

²⁴⁵ Ndipo alipomwambia shida yake, yeye akasema, “Bwana, na—naona ya kuwa Wewe ni nabii.” Akasema, “Tunajua ya kwamba ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya, lakini Wewe ni Nani?”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

Alirudi na kushuhudia na kumwambia kila mtu, “Mtu huyu aliniambia shida yangu. Hiyo si ndiyo ishara ya Masihi?”

²⁴⁶ Sasa, ingekuwa ni ishara ya Masihi kwako? Kama akija usiku wa leo, na, mimi hapa ni mwanamume, wewe ni mwanamke, tulikutana kwa mara yetu ya kwanza, kama angekuja, aniambie shida yako, ama jambo fulani kukuhusu ambalo unajua silijui, basi kama, kulifanya lisiweze kukosea, kama Yeye anaweza kukwambia jambo fulani ambalo umefanya, kitu fulani huko nyuma kile umefanya, ama umekuwa, kama Yeye anajua kile umekuwa, ama umefanya, mbona bila shaka anaweza kujua kile utakachokuwa, ama utakachofanya. Hiyo ni kweli?

²⁴⁷ Kwa mfano, kama, kama vile karama ya uponyaji, hapana shaka ila kwamba karama hiyo iko kote jengoni usiku wa leo, karama nyingi za uponyaji, sasa, kama ningekuwa nimekuleta hapa juu, nikakuwekea mikono, na kusema, “Haleluya! Mungu asifiwe!” baadhi ya ndugu zetu walio na karama za uponyaji, wangesema, “Utakuwa mzima. Mungu asifiwe! Endelea,” hiyo—hiyo ni kweli, ningeweza kuamini hilo, hakika. Ninaamini ya kwamba kila mmoja wa hao ndugu ana karama za uponyaji. Nafikiri Mungu atawafanya wawajibike kwa jinsi wanavyoitumia mara nyingi, lakini mimi, mwajua, wanapata pesa, na mambo kama hayo, lakini mimi—lakini mimi ninaamini ya kwamba ni karama za Mungu. Ninaamini, wangelikuwa na kicho zaidi kwazo, karama zingekuwa kubwa zaidi, na zitakuwa.

²⁴⁸ Lakini ninaamini kama mtu akija akakwambia alikuwa na karama ya uponyaji, alikuwa ni ndugu katika Kristo, sijali alikuwa wa kanisa gani, bado ningesema alikuwa ni mtu

wa Mungu, kama angeweke mikono yake juu yako, kasema, “Ninakuwekea mikono, wewe nenda nawe utapona,” ninaamini hilo, hakika. Lakini—lakini huenda ukawa na shaka kidogo kama utapona au la, kwa sababu inakubidi tu kuamini neno lake kwa hilo.

²⁴⁹ Lakini sasa, kama Kristo akija na kufunika hata hayo yote, arudi kule nyuma, na kuzungumza nawe juu yake, akwambie jambo fulani huko nyuma, anakuja hapa na kukwambia shida yako, na yale ambayo umefanya, basi unajua hilo halina budi kuwa na namna fulani ya nguvu, sivyo? Kwa sababu tumeinua mikono yetu mbele ya Biblia hii, na Mungu, na kusanyiko hili, hatufahamiani.

²⁵⁰ Lakini kama atanifunulia shida fulani uliyo nayo, jambo ambalo umefanya, jambo ambalo hukupaswa kufanya, ama jambo fulani unalojaribu kufanya, ama unajiandaa kufanya... Na huenda ikawa umesimama hapa kwa ajili ya mtu mwingine, huenda ikawa ni shida za kifedha, huenda ikawa ni shida za kinyumbani, sijui. Mimi—mimi tu... Wewe ni mwanamke tu aliyesimama hapo.

²⁵¹ Je, wasikilizaji wanaelewa hilo? Nje, mnaelewa hilo? Sasa, kama Yesu ni yeye yule jana na hata milele, kama anahitaji chochote, Yeye tayari amekiandaa kwa ajili yake, jambo pekee analoweza kufanya ni kujitambulisha Mwenyewe tu. Sasa, kama Yeye alikuwa amesimama hapa amevaa suti hii aliyonipa, asingeweza kufanya zaidi ya yale anayofanya sasa hivi, ingekubidi kuamini ya kwamba Yeye alifanya hivyo kwa ajili yako, maana ni kazi iliyomalizika. Sasa, nyote mnaamini hilo? Sasa, kama atafanya hivyo kwa mwanamke huyu, ni wangapi watakaokubali jambo hilo huko nje, na kuliamini?

²⁵² Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila nafsi humu ndani chini ya mamlaka yangu kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

Unaogua ngiri. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

Unaamini sasa?

²⁵³ Nilishika hilo, msiwazie hivyo. Sasa, mlidhani nilibahatisha hilo. Sikubahatisha. Msiwazie hilo. Sasa, mtauharibu tu mkutano, hamna budi kuamini. Ilitoka mahali fulani. Mnaona? Msiwazie hilo.

²⁵⁴ Yeye ni mtu mzuri, yeye ni Mkristo, ana roho nzuri, si mwomba lifti, wewe ni—wewe ni—wewe ni Mkristo, hiyo ni kweli, maana nilihisi ninii yako... Ungeweza kuwa mwenye dhambi. “Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!” Unaona? Roho yako inathibitisha kwamba wewe ni Mkristo.

255 Naam, una ngiri, una tezi ya ndani, una ugonjwa wa kibofu nyongo, na una ugonjwa wa moyo, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli, inua mkono wako.

Unaamini sasa?

256 Unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Unaamini Yeye anaweza kuniambia wewe ni nani? Lingekuwa ni jambo lile lile alilomwambia Petro? Bibi Roundtree, nenda nyumbani, amini kwa moyo wako wote nawe utakuwa mzima.

Sasa unaamini? Amini kwa moyo wako wote. Sasa, ilianza kutoka kwa wasikilizaji, hadi kwenu ninyi watu huko nje. Iweni na kicho kabisa, endeleeni tu kuomba.

257 Sasa, mama aliyesimama mbele yangu ni mgeni, yeye ni mdogo wa umri kuliko nilivyo mimi. Onyesho lingine, mwanamke, mwanamume wanakutana pamoja. Sijawahi kumwona maishani mwangu, lakini Mungu anamjua. Na kama hatufahamiani, mama, siyo? Hatufahamiani. Iweni tu na kicho kabisa sasa.

258 Sasa, sijawahi kumwona, simjui, basi kama Roho Mtakatifu atanifunulia jambo fulani kumhusu, hebu na awe ndiye mwamuzi kama ni kweli ama si kweli.

259 Yuko hapa kwa ajili ya shida ya kiroho, una shida za kiroho. Unaomba kwa ajili ya mtoto, pia, siyo? Msichana mdogo mwenye . . . ? . . . macho mabaya, hayupo hapa. Hiyo ni kweli. Una wifw yako hospitalini. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake? Ana nimonia. Nawe amini kwa moyo wako wote sasa, nenda, na umwamini Mungu, na uamini ataninii . . . ? . . .

260 Unaamini kwa moyo wako wote, moyo wako wote kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yu hai na anatawala? Sasa, lazima uamini kwa moyo wako wote. Sasa, je, vema, hilo linaridhisha shauku yako, “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu?” Sasa, ningewezaje . . . ?

261 Sasa, itakubidi kusema namna fulani ya nguvu zinafanya hivyo. Sasa, ukitaka kuziita nguvu za ibilisi, vema, endelea, na upate thawabu hiyo. Unaona? Lakini kama unaamini ni Yesu Kristo akilitumia tu Kanisa Lake, kulingana . . . Nililifafanua lote kwa Biblia, ya kwamba ni ahadi ya Mungu. Hiyo ni kweli, Kasisi? Ahadi ya Mungu. Unaona?

262 Sikilizeni, shida ya Wapentekoste leo, wengi wetu, tumemwona Mungu akitenda kazi sana hata ina—inakuwa ni kawaida kwetu. Mnaona?

Je, huyu ndiye mtu anayefuata? Sijarukwa na akili, lakini wakati mwingine Roho anavuta kote kwenye kusanyiko.

263 Kwa hiyo, sikujui, wewe hunijui, hatufahamiani. Kama Roho Mtakatifu anaweza kunifunulia jambo ambalo—ambalo unajua kama ni kweli ama si kweli, u—unaweza kushuhudia jambo hilo, kama ni kweli ama si kweli. Una udhaifu, ugonjwa

wa wasiwasi. Umekuwa hospitalini, nawe unasumbuliwa na udhaifu kutokana na upasuaji huo, na ilikuwa ni kansa, nao wakatoa viungo vyako vingi, sehemu ya matumbo, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Unaamini kwa moyo wako wote? Sasa angalia, unajua ya kwamba Kitu fulani hapa kinakujua, kwamba upako huo uko juu yangu sasa, na juu yako, hebu nikuwekee mikono.

Bwana Yesu, ninaombea uponyaji wake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Nenda sasa, usiwe na shaka. Nenda ukiamini kwa moyo wako wote.

Mwamini Mungu. Unaamini kwa moyo wako wote? Amini sasa, anza kuamini.

²⁶⁴ U hali gani, Dada? Mimi na wewe hatufahamiani, pia. Sijawahi kukuona, hujawahi kuniona, kwa hiyo hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana. Tulizaliwa maili nyingi mbalimbali, miaka tofauti, mara ya kwanza sisi—mara ya kwanza tumekutana. Amini tu sasa, endelea tu kuamini, usiwe na shaka.

²⁶⁵ Ulimgusa Yeye, shida yako ya shingo itakuacha, nawe utakuwa sawa. Amini kwa moyo wako wote, uliyeketi hapo, ukapangusa macho yako. Amini kwa moyo wako wote, Mungu atakuponya.

Aligusa nini? Yuko futi thelathini kutoka kwangu, aligusa Kitu fulani, alimgusa Kuhani Mkuu.

²⁶⁶ Mama huyo aliyeketi karibu nawe hapo ana shida na macho yake, anaugua ugonjwa wa jicho, pia. Akiamini kwa moyo wake wote, anaweza kuponywa, pia. Amina. Mnaona?

Amini, wala usiwe na shaka.

²⁶⁷ Unaugua ugonjwa wa moyo, una kuvuja kwa moyo. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya huo? Unaniamini mimi kama nabii wa Mungu, ama, mtumishi Wake? Jina hilo huwakwaza watu wakati mwingine. Unaamini? Unajaribu kuondoa tabia fulani, pia, sivyo? Kuchovya ugoro. Wewe, hivi unataka kuiacha sasa?

²⁶⁸ Ninakuamuru, ewe ibilisi, katika Jina la Yesu Kristo, kwamba umwache mwanamke huyu, achana naye, katika Jina la Yesu Kristo!

Nenda ukiamini, usiwe na shaka. Amini kwa moyo wako wote.

U hali gani? Hatufahamiani, Mungu anatumia sote wawili. Hiyo ni kweli?

Inaendelea tu kuvuta katika kusanyiko hilo, hapo nje.

269 Sikujui wewe, hatufahamiani. Wewe ni mdogo sana wa umri kuliko nilivyo mimi, tulizaliwa tumeachana kwa miaka mingi, umbali wa maili nyingi, na mara yetu ya kwanza kukutana.

270 Sasa, jambo hili lingeweza tu kuendelea usiku kucha, mnaona, bali ninawatakeni mtengeneze imani yenu pamoja na Mungu. Itatendeka kwa mwanamke huyu, je, nyote mtaamini kwa moyo wenu wote? Acha awe ndiye mwamuzi.

271 Nilikuwa nikitaka kusema, “Kama mtu yeyote hapa anamjua,” bali yeye hatoki kwenye mji huu, ametoka mahali pengine. Hiyo ni kweli. Lakini unaugua ugonjwa wa wasiwasi, ugonjwa wa mapafu, ugonjwa wa kike. Hiyo ni kweli. Bibi Olds, unataka kurudi nyumbani, uwe mzima? Nenda zako ukirudi, uwe mzima, katika Jina la Yesu Kristo.

272 Amini kwa moyo wako wote. Unaamini? Hebu na tumwabudu tu basi, na kusema, “Baba Mungu, tunakushukuru kwa msamaha Wako...?...Baba Mungu...?... tunakushukuru kwa sababu ya ninii Yako...?...katika Jina la Yesu.”

273 Tunaomba ya kwamba utawatia watu mafuta, Bwana, ili waweze kukujua Wewe kuwa ni Mungu wa kweli na aliye hai. Tunakushukuru, katika Jina la Yesu. Amina.

274 Vema. Vipi kama ningekwambia uliponywa ulipokuwa umeketi pale kitini? Je, ungeniamini? Vema. Endelea, na moyo wako hautakusumbua tena, unaweza kuponywa.

275 Una jambo lile lile. Unaamini ya kwamba Mungu atauponya moyo wako, na kukupa afya, pia? Kama wewe... Kama unaweza kuamini kwa moyo wako wote, basi nenda zako, useme, “Asante, Bwana Yesu,” na uamini kwa moyo wako wote.

Vema. Nenda ukale chakula chako cha jioni sasa, ugonjwa wako wa tumbo umekuacha, kwa hiyo endelea moja kwa moja.

Unaamini kwa moyo wako wote...?...Haidhuru—haidhuru una shida gani, mwamini tu Mungu.

276 Una tumbo lenye wasiwasi, bali Mungu atakuponya kama utaamini. Utaamini kwa moyo wako wote? Nenda zako, na useme, “Asante, Bwana.”

Kamwe hutalemazwa na yabisi kavu kama utamwomba Mungu akupe afya. Endelea, amini. Mungu akubariki.

277 Unaamini kwa moyo wako wote, kila mtu? Mungu angali anabaki... Vipi ninyi watu huko nje msio na kadi za maombi? Mnaamini? Mungu ni Mungu, sivyo?

278 Unasemaje hapo, jamani? Unataka kuacha hizo sigara na uache kuvuta sigara? Inua mkono wako, na umsifu Mungu. Hazitakusumbua tena.

279 Akiketi papo hapo karibu naye, yupo mwanamke upande huu, anayeniangalia, mwenye mkamba. Unaamini ya kwamba

Mungu atakuponya huo, mama? Unaamini kwa moyo wako wote? Inua mkono wako, na useme, “Ninaukubali.”

²⁸⁰ Vema, haya basi. Aligusa nini? Waligusa nini? Walimgusa Mwalimu, sio mimi. Baadhi yenu, mnataka kuamini?

Mama huyu aliyeketi papa hapa mwenye mzio, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, Dada? Vema, inua mkono wako, upate afya.

²⁸¹ Mama aliyeketi hapo akiniangalia hapa, aliyevaa kofia hii kubwa ya zambarau, anayeugua bawasiri huko nyuma, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, mama? Simama kwa miguu yako kama hiyo ni kweli. Mume wako aliyeketi papo hapo karibu nawe anaugua msongo wa mawazo. Simama kwa miguu yako, ndugu, na ukubali uponyaji wako. Mungu atakuponya.

²⁸² Mnaamini, kila mmoja wenu? “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.” Mnaona ninalomaanisha? Hao walikuwa ni watu wasio na kadi za maombi. Yuko hapa kuponya, sivyo? Sasa, kama unaamini Neno la Mungu kuwa kweli, Marko 16 ilisema hivi (Ni wangapi wenu ni waaminio? Inueni mikono yenu sasa.), Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Hiyo ni kweli? Je, Yeye alisema jambo hilo? Vema, kama ninyi ni waaminio, wekeaneni mikono, wekeaneni mikono.

²⁸³ Huu ndio wakati wa ibilisi kushindwa, papa hapa, kila mtu anaweza kuponywa. Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi. Mwombee jamaa uliyemwekea mikono. Ninyi hapa kwenye mstari wa maombi wekeaneni mikono. Nenda ukiamini. Amini kwa moyo wako wote.

²⁸⁴ Sasa, kila mmoja, kila mmoja, moja kwa moja wakati Roho Mtakatifu anapotenda kazi humu jengoni sasa, nisikilizeni, kama nimewaambia ukweli hapa, na Mungu amethibitisha ninawaambia kweli, kila mmoja wenu ameponywa, umeponywa tangu Yesu alipokufa kwa ajili ya uponyaji wako.

²⁸⁵ Sasa, wekeaneni mikono. Usijiombee mwenyewe, bali mwombee yule uliyemwekea mikono. Wekeaneni mikono sasa.

²⁸⁶ Sasa, wewe sema ombi hili nyuma yangu: “Bwana, naamini! Ninaamini ya kwamba mtu huyu ninayemwekea mikono yangu ataponywa. Ee Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa Milele, Mpaji wa kila karama njema!”

²⁸⁷ Shetani, ninakukemea, toka ndani yao katika Jina la Yesu Kristo! 

61-0118 Yesu Kristo Yeye Yule
Jana, Leo, Na Hata Milele
Kanisa La Kipentekoste La Lamar
Beaumont, Texas Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org